

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Udalali ya Tambaza, Abdaallahn Abeid (kulia), akijadiliana jambo na baadhi ya madalali wa mahakama, wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya sheria nchini, viwanja vya Mahamaka ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Igalula Auction Mart, Mwavua Kiguru na (wapili kulia) ni Mkurugenzi wa Active Auction Mart, Abdallah Makata. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia asema pesa zinatembea kortini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema bado Mahakama inakabiliwa na vitendo vya rushwa jambo ambalo linawanyima haki wasio nacho. Hivyo kusababisha malalamiko katika jamii.

Pia amesema yako malalamiko mengi kwa wananchi juu ya ucheleweshaji wa haki hususan kwenye masuala ya mirathi kwa wajane na migogoro ya ardhi.

Kutokana na hali hiyo, amewataka watendaji wa mahakama kutoa haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi na kutazama utu wa mtu.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini hapo kwenye kilele cha Siku ya Sheria nchini yenye kauli mbiu 'Zama za Mapinduzi ya Nne ya Viwanda: Safari ya Maboresho Kuelekea Mahakama Mtandao.'

Alisema rushwa bado iko katika ngazi ya mahakama na kusababisha mwenye haki kukosa haki na wasio na haki kupewa.

"Bado vijipesa pesa vinatembea. Inawezekana si katika ngazi za juu lakini huko ngazi za chini bado vijipesa vinatembea ambavyo vinasababisha mwenye haki anyimwe haki au kwa lugha rahisi niseme rushwa bado iko ndani ya mahakama," alisema.

Rais alisema Mahakama imepewa jukumu kisheria la kutoa haki na kuwataka watendaji wa idara hiyo kutoa haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi.

"Mwananchi anapoleta kesi yake mahakamani hajui chochote anategemea wakili kwa yule mwenye uwezo wa kuweka wakili lakini asiye na uwezo tunasema serikali tuna wajibu wa kumpa wakili. Lakini anayeshtakiwa ana uwezo wa kuweka wakili, sasa hawa kwa kutumia njia zao za kiufundi humnyima haki mwenye haki," alisema. "Angalia utu unakwambiaje uchukue fedha utelekeze utu wa mtu. Umetumia umahiri wa vifungu kumnyima mwenye haki, utu wako unakwambiaje? Niombe sana kuzingatia utu wa mtu," alisema.

Alipongeza kuanzishwa kwa Mahakama Mtandao kwa kuwa itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji mashauri na vitendo hivyo.

**AIPONGEZA TLS**

Rais Samia alikipongeza Chama Cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kwa kubadilika na kuendana na lengo la kuundwa kwake huku akiahidi kuwa serikali itashirikiana nao.

"Niwapongeze TLS kwa kujitambua na kwamba kwa sasa TLS inajitambua na inaelekea kwenye lengo la kuanzishwa kwake. Hapa katikati mnajua TLS mlichokuwa mnakifanya. Serikali iko pamoja nanyi na tutakwenda sambamba," alisema.

Kuhusu ombi la TLS la kuunganisha kada ya mawakili wa umma na binafsi, Rais Samia aliagiza washirikiane na Waziri husika kuangalia kama suala hilo linawezekana.

Awali, Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, alisema mfumo wa kuendesha mashauri kwa njia ya video umesimikwa katika vituo vya mahakama na baadhi ya Magereza na kwamba mashauri 17,979 yalisikilizwa na kuokoa Sh. bilioni 2.75 kwa mwaka kwa upande wa magereza, mawakili, mahakama na wadau wengine.

Pia alisema kwa sasa mahakama inafanya maboresho makubwa ya mfumo wake wa Menejimenti ya Mashauri ili uendane na mabadiliko ya kiteknolojia.

"Mfumo huu pamoja na mambo mengine hautaruhusu ufunguaji wa mashauri kwa njia ya kawaida na utakuwa na uwezo wa kutengeneza jalada la kielektroniki la mashauri," alisema. Prof. Juma alisema mfumo huo utashuka hadi mahakama za mwanzo na utafanikisha kuondokana na matumizi ya karatasi na kwamba wameanza kwa majaribio Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni na kupata mafanikio.

Pia alisema zimenunuliwa kompyuta mpakato (laptop) 1,388 kwa ajili ya majaji na mahakimu kwa ajili ya shughuli za mahakama hiyo ikiwamo kuandika hukumu na mwenendo wa mashauri.

"Mahakama ya Tanzania haiwezi kufumbia macho yale yanayoendelea katika jamii wala kubaki nyuma au kuendelea katika jamii wala kubaki nyuma au kuendelea kukumbatia mifumo ya kizamani ya uandishi wa mienendo ya mahakama kwa kuandika kwa mkono wakati akili bandia ipo kuwezesha kufanya kazi kwa wepesi na bila gharama," alisema.

Naye Rais wa TLS, Dk. Edward Hosea, alisisitiza mambo sita ikiwamo jamii kukubali na kuwa na elimu ya mabadiliko ya bongo bandia ambayo italeta maendeleo katika utoaji haki nchini.

Alisema lazima mifumo yote ya utoaji haki ifuatwe ili kutenda haki na kusisitiza utu wa mtu katika dhana ya utawala wa sheria.

Alitoa rai kwa vyombo vya dola kuzingatia utawala wa sheria ili haki itendeke kwa watu wote.

Dk. Hosea alisema chama hicho kitaanzisha vituo vya utoaji msaada wa kisheria nchini ili wananchi wasio na uwezo kifedha wapate nasaha za kisheria na kupunguza mashauri mahakamani.

Alisema uwekezaji wa Mahakama Mtandao utapunguza muda wa mashauri kukaa mahakamani, kupunguza gharama za uendeshaji kesi.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, alisema matumizi ya TEHAMA yanaziba mianya ya rushwa na kwamba ofisi yake inaendelea kuboresha mifumo ili isomane na mingine.

"Mahakama mtandao itafanikisha utoaji haki kwa wakati, kuanzia juzi yamefunguliwa mashauri 301 kati ya hayo 296 yalifunguliwa kwa mtandao na matano ndio yaliyofunguliwa kwa mkono, pia kuanzia Januari hadi leo kati ya mashauri 5,447 yaliyofunguliwa mashauri 5,235 yalifunguliwa kielektroniki na mashauri 212 tu yalifunguliwa kwa njia za kawaida," alisema.

# Serikali yabanwa Bwawa la Nyerere

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina, ameihoji serikali juu ya kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la Nyerere, huku akieleza mawaziri wamekuwa na majibu kinzani kwa jambo moja.

Aidha, alitaka kujua kauli moja ya serikali kuhusu mgawo wa umeme na sababu za kuwapo.

Akiuliza swali la nyongeza baada ya kujibiwa swali la msingi alisema walipokuwa kwenye Kamati ya Bajeti Novemba mwaka jana, Waziri alieleza sababu za mradi kuchelewa ni mkandarasi kukaidi muundo uliowekwa na wataalamu wa kujenga mahandaki matatu kwa ajili ya kuchepusha maji, lakini alijenga moja, hivyo kuchelewesha kazi.

"Mbele ya Kamati sababu za UVIKO-19 zilikataliwa na majibu haya yako kwenye kumbukumbu za Bunge kwenye kamati, lakini leo hii wamekuja na majibu mengine," alisema. "Kwa sababu haya majibu yanakanganya kwenye kamati waliyakataa majibu kwamba hayana ukweli wakasema majibu sahihi ni uzembe na atapigwa faini kwa kuchelewesha mradi wa Watanzania wanaousubiria.

"Sasa Waziri atuambie kamati ni sehemu ya Bunge, na hapa wamekuja na majibu mengine na ushahidi wa kumbukumbu za Bunge upo, nini majibu ya serikali ya kucheleweshwa mradi huu kwa sababu majibu mawili yameshatolewa," alisema na kuongeza:

"Kwa majibu haya yaliyotolewa mradi wetu huu wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere hauwezi kukamilika kama mkataba unavyosema."

Katika swali la msingi, Mpina alitaka kujua sababu zilizosababisha kuchelewa kukamilika kwa ujenzi huo, kwa nini mkandarasi ameshindwa kujaza maji kwenye Bwawa kufikia Novemba 15, 2021 kama ilivyokuwa imekubalika na hatua zilizochukuliwa kutokana na ucheleweshwaji huo.

**MAJIBU YA SERIKALI**

Akijibu , Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema muda wa kukamilika kwa mradi kimkataba ni Juni, mwaka huu, na kwamba hiyo tarehe haijafika.

Alifafanua kuwa ili bwawa hilo lianze kujazwa maji, ni sharti liwe limejengwa kufikia kimo cha mita 95 juu ya usawa wa bahari, kazi ambayo imekamilika.

"Ilitakiwa handaki lililojengwa kuchepusha maji ya Mto Rufiji kuzibwa. Kazi ya kuziba/kufunika handaki kwa kutumia vyuma maalumu vizito ilihitaji mfumo (maalum wa kudumu) wa mitambo ya kubebea milango hiyo (Hoist Crane system) kuwapo katika eneo la mradi,"alisema na kuongeza:

"Mfumo huo unatengenezwa mahsusi kwa ajili ya kazi hii na kazi inapoisha crane hizo huondolewa na hautumiki kwa kazi nyingine. Mitambo hiyo ilichelewa kufika kwa wakati kutokana na viwanda kufungwa na safari za meli kuathiriwa kutokana na UVIKO 19. Milango na mtambo wa kubebea imefika na kazi za kuifunga zinatarajiwa kukamilika Machi, mwaka huu."

**MGAWO WA UMEME**

Katika swali la pili la nyongeza, Mbunge huyo alihoji majibu kinzani ya viongozi hao kuhusu kuwapo kwa mgawo wa umeme nchini na sababu zake.

"Kata kata ya umeme inayoendelea na mgawo unaoendelea hivi sasa mwanzo tulielezwa sababu ni matengenezo ambayo hayakufanyika kwa miaka mitano na kuwa wako kwenye matengenezo, baada ya muda mfupi tukaambiwa kwa sababu ya mabwawa ya kufua umeme kukauka kutokana na mifugo na ukaidi wa binadamu," alisema na kuongeza:

"Sasa hivi tena TANESCO wanasema hakuna mgawo wa umeme baadaye TANESCO wanatangaza mgawo wa umeme. Sasa tuelezwe na serikali kwa sababu katakata umeme inaathiri Watanzania, viwanda vinafungwa, wananchi wapo kwenye dhiki kubwa, huduma za afya zimevurugika, huduma za maji zimevurugika kwa ujumla taifa liko kwenye hali ngumu ya ukosefu wa umeme, tunataka waseme nini kinasababisha katakata ya umeme."

Katika majibu yake, Byabato alisema "Do not cross the river before you reach there' (usivuke mto kabla ya kuufikia) muda utakapofika kama mradi hautakamilika hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa mkataba kwa atakayesababisha ucheleweshaji.

Kwa mujibu wa Byabato, , TANESCO haikati umeme kwa kuwa hakuna aliyeajiriwa kwa ajili ya kukata umeme, bali mifumo inafanyakazi kulingana na mazingira na mitambo ikizidiwa na matumizi inakata umeme na wanapobaini tatizo wanawasha.

## HABARI KITAIFA

# Mlinzi wa shule auawa

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MLINZI wa Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Winning Spirit iliyoko eneo la Terat jijini Arusha, Issa Dinaoh (57), ameuawa kikatili na watu wasiojulikana baada ya kutenganishwa kichwa na kiwiliwili na kisha wauaji kuondoka na kichwa chake.

Shule hiyo inamilikiwa na Meya wa Jiji la Arusha, Maximilian Iranqhe.

Jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Joshua Mwafilango, alithibitisha kuwa mlinzi huyo aliuawa usiku wa kuamkia juzi huku wauaji wakiondoka na kichwa chake muda mfupi baada ya kutekeleza mauaji hayo.

Kwa mujibu wa Mwafilango ambaye ni Mkuu wa Upelelezi wa Mkosa ya Jinai wa Mkoa wa Arusha (RCO), hadi kufikia sasa wanamshikilia mlinzi mmoja aitwaye Raymond Mollel kwa uchunguzi zaidi, huku akidai kuwa katika uchunguzi wa awali mlinzi huyo amekiri kuhusika na tukio hilo.

"Tunamshikilia huyu mlinzi maana katika eneo hili la shule lina walinzi wawili ambapo mmoja ndiyo huyu marehemu na mmoja huyu tuliyenaye ambaye amekiri kuhusika, tunaendelea na mahojiano kufahamu zaidi chanzo cha mauaji haya," alisema.

Aliongeza kwa baada ya msako wa kimyakimya, makachero wa polisi pia walifanikiwa kupata kichwa cha marehemu huyo.

Kamanda Mwafilango alisema mwili umehifadhiwa katika Chumba cha Kuhifadhi Maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Alipoulizwa kuhusu tukio hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Olkung'u ulioko Kata ya Terati, Daud Topiwo, alisema aliitwa na wananchi wake kwenda eneo la tukio kuona kiwiliwili cha mlinzi huyo jana asubuhi na alipofika alishangaa kuona kikiwa bila kichwa.

Alisema mlinzi huyo ni wa siku nyingi katika eneo hilo linalomilikiwa na meya na wamemzoea, hivyo kitendo kilichofanywa na watu wasiojulikana ni cha kinyama na kibaya.

Alisema wao kama wananchi wanaliachia Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi na utaalamu walionao kubaini wahalifu wa tukio hilo.

"Ila mimi kama kiongozi wa mtaa huu nitaitisha mkutano wa hadhara na wananchi wangu ili tuweke mikakati ya kuimarisha ulinzi na usalama wa eneo letu," alisema.

Aliwaomba wananchi kutojiingiza katika vitendo hivyo vya kinyama na visivyofaa kwa binadamu kwa kuwa "Mungu yupo na malipo yapo hapa duniani".

Mmiliki wa eneo hilo, Meya Iranqhe, alisema amesikitishwa na kitendo hicho cha kinyama na kukiri kuwa aliyeuawa ni mmoja wa wafanyakazi wake.

"Lakini siwezi sema mambo mengi zaidi, tuliachie Jeshi la Polisi lifanye kazi yake,"




Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (kushoto), akipokea zawadi ya jarida linalozungumzia masuala mbalimbali ya Marekani, kutoka kwa Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, baada ya mazungumzo kuhusu ushirikiano yaliyofanyika jijini Dodoma, jana. **PICHA: WMNN.**

# 27 mbaroni kwa tuhuma wizi lori lililopata ajali

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam linawashikilia watu 27 kwa tuhuma za kuiba saruji mifuko 368 kwenye matukio mawili ya wizi wa magari eneo la Mbagala Misheni, Wilaya ya Temeke.

Kamanda wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, alibainisha hayo jana mkoani humo alipozungumza na waandishi wa habari na kusema kuwa watu hao walikamatwa katika matukio yaliyotokea Januari 4 na 5, mwaka huu wilayani humo.

Alisema imezuka tabia ya baadhi ya watu pindi ajali inapotokea, badala ya kusaidia majeruhi, wanajihusisha na vitendo vya uhalifu.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi lilibaini kuwapo kwa matukio hayo na baada ya ajali lilifanya msako wa nyumba zilizokuwa karibu na tukio na kuwakamata watu hao pamoja na mifuko ya saruji 368.

Pia alisema wamekamata pikipiki tatu na bajaji ambazo wakati wa matukio hayo zilitumika kusafirisha saruji hiyo.

Alisema watuhumiwa wamehojiwa na upelelezi unakamilishwa ili wafikishwe mahakamani.

"Hatutasita kuwashughulikia kisheria watu wote ambao kwa sasa wamekuwa wakikimbilia matukio ya ajali badala ya kuokoa watu na mali wanageuka kuwa wahalifu," alionya.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linaendelea kuwasaka wahusika wote mpaka mtu wa mwisho aliyehusika katika wizi wa mali hiyo.


## NOTISI KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **MASE INTERNATIONAL LIMITED, BROVITAS COMPANY LIMITED, JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER, INDEPENDENCE AGENCIES & COURT BROKER NA HOLLYNESS & RESPISHERS COMPANY LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| NOTISI KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|
| MASE INTERNATIONAL LIMITED | | |
| JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| DAUD LIFU MREFU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | CHOMETE- TARIME |
| ANDREA .N. MAJANGA | KIWANJA CHENYE HATI KIWANJA NO.597, KITALU NN, ILIYOPO, UGWETO-SHINYANGA. | UGWETO-SHINYANGA |
| BROVITAS COMPANY LIMITED | | |
| JOHN STEPHEN MAKUNDI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MSHANGANO-SONGEA |
| GEORGE GERLOD MGAYA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MKUZO-SONGEA |
| AJIBU HEMED AMAN | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MSAMALA MAKING'INDA-SONGEA |
| ELIZABET CLEMENCE MZUMALA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MKUZO-SONGEA |
| LOIRUCK EMANUEL LOSARU | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | RUHUWIKO NA MWENGEMSHINDO-SONGEA |
| FELIX ANDREA NJAU | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MKUZO-SONGEA |
| JABU MOHAMED ALLY | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | RUVUMA-SONGEA |
| GERLAD JOSEPH NCHIMBI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MALIASILI-SONGEA |
| PETER PETER MAPUNDA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | RUVUMA-SONGEA |
| ASHA O NJADI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | LIZABONI-SONGEA |
| INDEPENDENT AGENCIES &COURT BROKER LTD | | |
| MARIESTA A KIMARIO | NYUMBA YENYE HATI KIWANJA NO 492, KITALU E-MSARANGA MOSHI | MSARANGA-MOSHI |
| RACHAEL BARIKIEL MASSY | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | WASOMALI, HAI-MOSHI |
| HOLLYNESS & RISPERSHERS COMPANYLIMITED | | |
| AYUB M SUMUN | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | VINGUNGUTI-MBEYA |
| DAUDI A MWAIBOFU | NYUMBA YENYE HATI KIWANJA NO.444, BLOCK M | ITIJI-MBEYA |
| ELIAS K MWAKASEKELE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | VETA-MBEYA |
| JOSINA COMPANY LIMITED& AUCTIONEER | | |
| INNES L KALINJUNA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KASHENYE-BUKOBA |
| CLEMENT KIHAMA MANYALA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIBETA-BUKOBA |
| EDIGAR CHARLES DAUDI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | ITAWA-BUKOBA |
| GADAU AUCTION MART& COMPANY LIMITED | | |
| SUBIRA ISSA SADALA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MKUNDI-MOROGORO |
| JOSEPH MABULA MAIGE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MJI MPYA-MOROGORO |
| PETER JOHN UISO | GARI AINA YA TOYOTA YENYE USAJILI NO.T 184 AHD | MOROGORO TOWN |
| THECLA R KALAGE | GARI AINA YA BREVIS YENYE USAJILI NO.T 952 CLX NA NISSAN MISTRAL YENYE USAJILI NO.T549 AUM | MOROGORO TOWN |
| ANGEL B MPEPO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. 1203 SQ | KAYENZI-MOROGORO |
| ABDALA AMINI MUANGA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO NA MASHINE ZA KUKOBOA | TUSHIKAMANE-MOROGORO |
| ISSA R MMBAGA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | LUKOBE KAMBI TANO-MOROGORO |
| EMANUEL F MARWA | GARI AINA YA SCANIA YENYE USAJILI NO.T252 BZD | MOROGORO TOWN |
| ALLAN ELIAPENDA MAKUNDI | VIWANJA VIWILI VYENYE MKATABA WA MAUZIANO | KILAKALA & MKUNDI - MOROGORO |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mase International Limited**
**S.L.P 6197 Mwanza**
**Namba Za simu: 0743 885084/0710885084**
**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji.**
**Josina Company Limited and Auctioneer**
**S.L.P 40855 MWANZA**
**NAMBA ZA SIMU; 0713203040/ 0768203040**
**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Brovitas Company Limited**
**S.L.P**
**Songea**
**NAMBA ZA SIMU: 0628555260**

**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Hollyness & Respishers Company Limited**
**S.L.P**
**Dar es Salaam**
**Namba za simu; 0762058614**
**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Gadau Action Mart & Company Limited**
**S.L.P 40855**
**NAMBA ZA SIMU: 0752051755**
**Na**
**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Mobile#: 0768790399, 0754774949**

166879

# Corona yagharimu maisha ya mawakili

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) Mkoa wa Njombe kimesema tangu kulipuka kwa ugonjwa wa UVIKO-19, mawakili 65 nchini wamefariki dunia huku kikishuhudia athari kubwa kiuchumi kwa kada hiyo.

Mratibu wa TLS Mkoa wa Njombe, Innocent Kibadu, alibainisha hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Sheria yaliyofanyika viwanja wa mahakama mjini hapo.

Alisema kuwa athari za UVIKO-19 hazikuishia tu kuchukua maisha ya wapendwa wao, bali pia zimeathiri kwa kiasi kikubwa hali ya kiuchumi kwa mawakili binafsi na familia zao.

"Athari za UVIKO-19 ni nyingi ikiwa ni pamoja na watu kupoteza maisha, kudhoofika mwili, kupunguza kasi ya kufanya kazi, kuathiri uwezo wa taasisi mbalimbali zinazojitegemea na za umma kujiendesha kiufanisi na kurudisha nyuma mipango ambayo kila taasisi imejiwekea," alisema Kibadu.

Aliongeza: "Sisi kama chama tumepoteza mawakili wenzetu wapatao 65."

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Marwa Rubirya, Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema jamii inapaswa kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 kuwa kuwa ni salama kwa binadamu.

"Chanjo ipo kwenye vituo vyote vya kutolea huduma, chanjo hii ni salama, nendeni mkachanje ili muwe salama," alihimiza Kasongwa.

Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Njombe, Liadi Chamshama, alisema uanzishwaji wa mahakama ya kimtandao utasaidia kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani.

"Mbali na kupunguza mrundikano wa watu, pia itasaidia ufanisi na kupunguza uwapo wa mashauri mengi yanayoletwa mahakamani kwa mujibu wa sheria," alisema Chamshama.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, akiwaonyesha waandishi wa habari, mkoani humo jana, gari aina ya Toyota IST la dereva Taxi, Respikius Anastaz, aliyeuawa kwa kunyongwa na kamba na kutobolewa macho na abiria waliomkodi Januari 26, mwaka huu, katika eneo la Buzuruga, Wilaya ya Ilemela na kudaiwa kufanyia mauaji hayo wilayani Sengerema. **PICHA: ROSE JACOB**

# Utendaji kazi serikalini kupimwa kielektroniki

**Na James Mwanamyoto,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama amesema serikali inaboresha Mfumo wa Uwazi wa Kupima Utendaji Kazi wa Taasisi, maarufu kama Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi katika ngazi ya Taasisi za Umma kuwa wa kielektroniki ili utumike kupima utendaji kazi wa taasisi za umma nchini.

Akizungumza jana ofisini kwake jijini hapa, Mhagama alisema mfumo huo wa kielektroniki utawezesha makubaliano ya kimaandishi kati ya serikali na taasisi za umma kuhusu malengo ambayo taasisi husika itayatekeleza katika kipindi cha mwaka mmoja.

"Malengo yaliyomo ndani ya mkataba yatakuwa na vigezo, shabaha na viashiria vitakavyotumika kupima utendaji kazi wa taasisi kila mwisho wa mwaka. Mkataba huu unalenga kuimarisha utendaji unaojali matokeo, kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kuongeza uwajibikaji wa viongozi katika taasisi za umma," alisema Mhagama.

Aliongeza kuwa mfumo huo wa kielektroniki ukikamilika utatumika kulinganisha na kushindanisha utendaji wa taasisi na kutoa tuzo za utendaji bora kwa taasisi zenye utendaji mzuri kila mwaka.

Kuhusu faida za mfumo huo, Mhagama alisema utaongeza uwajibikaji katika utekelezaji wa sera, mikakati na vipaumbele vya taasisi, sekta na taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuboresha utoaji huduma kwa umma, kuimarisha utamaduni wa utendaji unaojali matokeo na kuleta matumizi bora ya rasilimali za umma.

Pia aliwataka makatibu wakuu na watendaji wakuu wote wa taasisi za umma kuendelea kusimamia utekelezaji wa mfumo huu kikamilifu na kuhakikisha wanatenga bajeti kwa ajili ya kusimamia utekelezaji katika taasisi wanazoziongoza.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejipanga vizuri kujenga na kusimamia mifumo yenye tija kupitia sekta ya Utumishi wa Umma.

# Kesi kina Sabaya yaahirishwa kidijitali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imeahirisha kusikilizwa kwa shauri la aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, kwa kuwa tarehe ya usikilizwaji wa kesi hiyo imeingiliana na kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria.

Hakimu wa mahakama hiyo, Patricia Kisinda, aliahirisha kesi hiyo kwa njia ya mtandao jana akiwa kwenye maadhimisho ya Wiki ya Sheria kiwilaya katika Mahakama ya Wilaya ya Monduli.

"Ninaahirisha kusikiliza shauri hili hadi hapo kesho (leo) Februari 3, mwaka huu tutakapoendelea na usikilizwaji wa kesi majira ya saa 3:30 asubuhi," alisema Hakimu Kisinda.

Sabaya ambaye ni shahidi wa pili wa upande wa utetezi kwa mshtakiwa wa kwanza, anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 27 katika mahakama hiyo.

Mbali na Sabaya washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu(26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya(31) wanakabiliwa na mashtaka matano yakiwamo la kuongoza genge la uhalifu, kujihusisha na vitendo vya rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na utakatishaji wa fedha.

Akizungumza mahakamani huko jana, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Janeth Sekule, alidai kwamba shauri lilikwenda kwa ajili ya kusikilizwa lakini aliomba liahirishwe kwa kuwa muda ulikuwa umekwenda na hakimu alikuwa kwenye maadhimisho ya Wiki ya Sheria katika Mahakama Wilaya ya Monduli.

Wakili wa Upande wa Utetezi, Mosses Mahuna, alidai walikuwa tayari kwa ajili ya usikilizwaji wa shauri lakini hawakuwa na pingamizi la kuahirishwa kusikilizwa kesi hiyo.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu linalowakabili washtakiwa wote, la pili ni kujihusisha na vitendo vya rushwa, likimkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake na la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa linalomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linalomkabili Sabaya peke yake na shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha linalowakabili washtakiwa wote saba.

# MATANGAZO


SOS CHILDREN'S VILLAGES TANZANIA

## KUWA SEHEMU YA MSISIMKO WA "FAMILIA YA SOS"

Je unataka kuwahamasisha watu na wakati huo huo kuchangia katika jamii yenye tija, jumuishi na endelevu zaidi? Tuna nafasi kwa ajili yako ili uwe sehemu ya familia kubwa ya shirika la SOS, kama Mjumbe wa Kitaifa wa Chama cha Hiari. Kwa sasa tuko katika mchakato wa kuchagua Wanachama wa Chama cha Kitaifa. Ungana nasi kwenye dhamira yetu ya kusaidia watu wenye uhitaji. Njoo ushiriki kwenye safari ya kusisimua ya kubadilisha maisha kuwa bora zaidi.

Shirika la SOS Children's Villages ni shirika linalolenga watoto, lisilo la kiserikali linalotoa matunzo na msaada kwa watoto ambao wamepoteza malezi ya wazazi au walio katika hatari ya kupoteza malezi ya wazazi wa familia zao halisi. Shirika la SOS Children's Villages, Tanzania, ni mwanachama wa shirika la Kimataifa la SOS Children's Villages, ni moja ya shirika kubwa lisilo la kiserikali na lisillo la kidini linalofanya kazi na jumuiya, wadau na mataifa mbalimbali ili kuhakikisha haki za watoto wote zinatimizwa katika kila jamii. Nchini Tanzania, kuna matawi manne ya shirika la SOS Children's Villages ambayo yako chini ya Programu ya Malezi ya Familia ya shirika la SOS zinazotekelezwa Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar (Unguja). Programu zingine ni pamoja na; Uimarishaji wa Familia, Utetezi, Elimu na Uwezeshaji wa Vijana. Shirika la SOS Children's Villages Tanzania linatekeleza programu zake katika maeneo sita; Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Mwanza, Pemba na Unguja.

**Maono yetu:**
Kila mtoto alelewe kwenye familia na kukua kwa upendo, heshima na usalama

**Dhamira yetu:**
Tunajenga familia mbalimbali kwa ajili ya watoto wenye uhitaji, tunawasaidia kuwajengea mustakabali wao na baadaye tunashiriki katika uendelezaji wa jamii zao.

**Maadili Yetu**
- Ujasiri - Tunachukua hatua.
- Ahadi - Tunatimiza ahadi zetu.
- Imani - Tunaaminiana.
- Uwajibikaji - Sisi ni washirika wa uhakika.

**Dhamira ya jukumu:**
Wanachama wa Chama cha Kitaifa watakuwa na jukumu la kufanya uchaguzi na upigaji kura kwa ajili ya kujaza nafasi za uongozi wa shirika, kulisaidia shirika katika kutimiza malengo yake ya kimkakati, kupokea taarifa za maendeleo ya shirika kwa njia yoyote ya mawasiliano, kuhudhuria mkutano mkuu kikamilifu na kushiriki katika shughuli zote za shirika, kadiri zitakavyohitajika.

**Majukumu makuu ya wanachama:**
- Kupokea na kuidhinisha ripoti za Mwenyekiti.
- Kuidhinisha taarifa za fedha zilizokaguliwa.
- Kupendekeza na kuchagua wajumbe wa bodi wa kitaifa.
- Kuteua na kuidhinisha wakaguzi wa hesabu kwa mwaka ujao.
- Kuchagua na kuteua kamati huru ya uteuzi ambayo itasajili wanachama wapya.
- Kushiriki katika shughuli za chama za kitaifa baada ya kupewa mwaliko.
- Kuidhinisha mabadiliko katika sheria na kuidhinisha shughuli kubwa kama vile muungano na utanguzi wa shirika.

**Sifa, maadili na mtazamo binafsi:**
- Mshiriki anayethamini michango ya wengine, anayeweza kutengeneza mazingira ya uungwaji mkono na salama kwa wengine katika shirika.
- Mwenye uwezo wa kukabiliana na matatizo, mwenye uthabiti na ustahimilivu uliothibitishwa wakati wa kukabiliana na matatizo ya ndani au nje ya shirika.
- Mtu anayefikiri "Nje ya boksi'.
- Mwenye uwezo wa kufanya maamuzi ambayo yatasaidia shirika kusonga mbele na kustawi.
- Mtu asiye na rekodi za uhalifu.

**Mitazamo:**
- Mwenye shauku na mbinu za ufumbuzi/utatuzi wa tatizo zenye kuleta matokeo chanya.
- Mwenye utayari wa kuchangia utaalamu, uzoefu na kujua jinsi ya kulisaidia shirika.
- Mwenye uwezo wa kuhisi maono ya mwingine ambayo yanaongeza ushirikishaji na uwezeshaji.
- Mwenye imani thabiti kuhusu mfumo wa haki dhidi ya mfumo kandamizi.
- Mwenye shauku kubwa kuhusu mbinu za ubunifu na uongozi wa mabadiliko kwa ajili ya utendaji bora.

**Vigezo vya chini vinavyohitajika kwa wanachama:**
- Anapaswa kulifahamu shirika la SOS Children's Villages na awe ameshaliunga mkono hapo kabla, au awe tayari kuwa rafiki wa shirika la SOS.
- Anapaswa kujitolea kwa ajili ya maono, dhamira na maadili ya shirika la SOS Children's Villages.
- Anapaswa kuwa mtu mwenye uadilifu wa hali ya juu na mwenye uwezo wa kuchunguza na kutoa ushauri na ufumbuzi wa changamoto za shirika.
- Anapaswa kuwa mtu ambaye hana mgongano wa kimaslahi unaoweza kukiuka katiba ya shirika, sheria za nchi na kanuni.
- Anapaswa kuwa na uwezo katika mojawapo au maeneo kadhaa kati ya yafuatayo: haki za watoto na mbinu za malezi ya watoto, masuala ya kijamii na watoto nchini, na uendeshaji wa jumla wa mashirika yasiyolenga kutengeneza faida.
- Anapaswa kuwa mtu ambaye atajitolea muda wa kutosha kwa ajili ya shughuli za shirika kuunga mkono mwelekeo wa jumla wa kimkakati.
- Mtu mwenye uwezo usiotiliwa shaka wa kuwakilisha masilahi ya msingi ya shirika kote ndani na nje ya shirika.
- Mwenye uelewa mkubwa sana kuhusu ulinzi wa mtoto ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu sera na sheria za viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Ni lazima awe na ufahamu wa jumla wa mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto.
- Anapaswa kuwa na uwezo wa kulipa ada ya mwaka ya uanachama.

**Kiwango cha chini cha ujuzi na sifa zinazohitajika**:
- Aliyehitimu kuanzia kidato cha nne hadi ngazi ya chuo kikuu.
- Awe na uzoefu wa kazi uliothibitishwa wa kufanya kazi na kushiriki katika programu mbalimbali za kusaidia makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.
- Awe na uzoefu wa kutekeleza programu/miradi mbalimbali inayohusiana na watoto.
- Awe na rekodi nzuri ya kufanya kazi za programu jumuishi.
- Awe na ujuzi thabiti na uwezo wa kuwasiliana na watu wa chimbuko mbalimbali.
- Awe anajua lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na uwezo wa kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza.
- Awe na uwezo wa kutii sera yetu ya ulinzi wa watoto.
- Awe na uwezo wa kulipa ada ya uanachama ya kila mwaka ambayo ni sawa na Dola za Kimarekani 100.00
- Awe na umri wa kuanzia miaka 35 – 50

Shirika la SOS Children's Villages Tanzania lina sheria kali za ulinzi wa mtoto na sera ya kutovumilia kabisa unyanyasaji wa kijinsia, unyonyaji na unyanyasaji mahali pa kazi. Sambamba na uwezo wa kitaaluma, uajiri, uteuzi na maamuzi ya kuajiri litaweka msisitizo unaostahili katika kutathmini ulinganifu wa maadili ya waombaji na uchunguzi wa kina wa historia, michakato ya uchunguzi wa taarifa za polisi.

**Jinsi ya Kutuma Maombi:**
Kama unatamani kuwa sehemu ya harakati za kiulimwengu za kuwapa watoto makazi yenye upendo tafadhali wasilisha Wasifu wenye ukurasa 1 ambao unaelezea umri, sifa za kitaaluma, uzoefu na barua fupi ya motisha yenye angalau anwani za watu (3) wanaoweza kuwasiliana nao, maombi. yanapaswa kutumwa kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe **Member.Association@sos-tanzania.org.**

Maombi yote yanapaswa kuwasilishwa kabla ya tarehe 17 Februari 2022 na waombaji waliochaguliwa tu ndio watawasiliana nao.

166887



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA MIRADI YA UWEKEZAJI WA KIJAMII KWA MAKUNDI YA KIKABILA YANAYOGUSWA NA MRADI WA EACOP
## KUMBUKUMBU NAMBA. 0010007446

TotalEnergies East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi, inaalika taasisi (kampuni au AZAKI) zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kubuni na kutekeleza mpango wa uwekezaji wa kijamii kwa makundi ya kikabila yanayoguswa na Mradi.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unatafuta huduma kutoka kwa shirika lenye uzoefu wa kutosha, (Kampuni au AZAKI inaweza kuitikia kwa kuonyesha nia ili kubuni na kutekeleza mipango ya uwekezaji wa kijamii na kujenga uwezo kwa jamii zilizochaguliwa za makundi ya kikabila yaliyoguswa na Mradi katika mikoa ya Tabora, Manyara, Dodoma na Tanga.

Muundo wa programu utalenga kutoa msaada wa uboreshaji wa maisha kimila (wafugaji au wawindaji) wa makundi haya ikijumuisha lakini sio tu usimamizi wa ardhi, afya ya mifugo na ufugaji, mahitaji maalum ya wanawake bali unapaswa kuundwa kwa njia ambayo inazingatia mahitaji ya uhifadhi na uendelevu.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**
Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuleta maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:
- Uthibitisho wa uzoefu katika kusaidia makundi ya kikabila yaliyo katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na kubuni na kutoa programu za maendeleo kwa jamii na jumuiya hizo.
- Uthibitisho wa usajili na leseni ya sasa ya biashara kwa makampuni au AZAKI kwa Asasi zisizo za kiserikali (AZAKI).
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kazi data ya EWURA ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha nia ya maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani.

Taasisi yenye nia, ambayo ina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu inapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11 alasiri** saa za Afrika Mashariki (EAT), tarehe **Februari 16 2022 .** Kichwa cha Barua pepe kiwe **0010007446.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni au AZAKI) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taaisi zenye nia. Mwaliko kwa taasisi kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenye vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya UtunzajiwaTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

166867

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tutengeneze umeme bila kuuzima kwanza

**SEHEMU** kubwa ya Tanzania kwa sasa inakumbana na athari za kukatika kwa umeme kutokana na mgawo uliotangazwa na serikali, ambao utachukua siku 10.

Katika utekelezaji huo, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Jumatatu lilitoa ratiba ya mgawo wa umeme kuanzia juzi hadi Februari 10, mwaka huu, ambapo mikoa 19 ya shirika hilo imetajwa, huku nishati hiyo ikikosekana kwa saa 16 kwa siku kuanzia saa 02 asubuhi hadi saa 06 usiku.

Hata hivyo, wakati wakazi wa maeneo ya mikoa ya TANESCO ambayo itaathirika ni Dar es Salaam (Temeke, Kinondoni na Ilala), Kilimanjaro na wilaya zake, Arusha, Mara, Mbeya, Manyara, Njombe, Morogoro, Mwanza, Singida, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Tanga, Tabora, Dodoma, Songwe, Iringa na Geita, mgawo huo, maeneo nyeti kama ya Jeshi na hospitali hayataguswa. Mikoa ya TANESCO ambayo haitaathirika kwa mgawo ni Bukoba, Katavi, Kigoma, Lindi, Mtwara, Pemba Kaskazini na Kusini, Rukwa, Simiyu, Zanzibar, Unguja Kaskazini na Magharibi.

Lengo la kufanyia matengenezo miundombinu ya umeme ni zuri na linakubaliwa na kila mmoja, kwa kuwa ni kuiboresha, hivyo kuongeza ubora wa huduma kwa watumiaji wa nishati hiyo.

Jumatatu ikiwa siku moja kabla ya mgawo huo kuanza juzi ambao unachukua saa 16 kwa siku kwa mujibu wa ratiba ya shirika, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alitembelea kituo cha kupozea umeme cha Kunduchi mkoani Dar es Salaam na kutoa ufafanuzi kuhusiana na suala la kukatika kwa umeme katika maeneo yaliyoorodhesha, akisema kwamba hakuna eneo umeme utakatika kwa siku tatu mfululizo.

Alisema wanaendelea na maboresho na kwamba wamejipanga kujua matatizo, majawabu yake na kuwa na mipango ya kuitatua. Alieleza kuwa Tanzania nzima wanajua kila mahali tatizo ni nini, majawabu ni nini na tarehe ya kuyatatua ni lini, hivyo kwa sasa wapo kazini kutekeleza. Kwamba katika zoezi la kuongeza mitambo ya uzalishaji wa umeme, kutakuwa na uhitaji wa gesi zaidi, akifafanua kuwa hilo linalazimu maboresho kufanyika katika visima vya gesi.

Kwa mujibu wa Chande, wakati maboresho hayo yanafanyika, watatumia siku 10 kufanya uboreshaji wa miundombinu ya umeme, huku akieleza kuwa hilo litasababisha umeme kukatwa kwa baadhi ya maeneo na siyo nchi nzima kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakisema. Pamoja na mgawo kukusudia kufanyia marekebisho miundombinu, tunaona kuwa utaathiri kwa kiwango kikubwa watumiaji hususani watu waliojiajiri kwenye sekta binafsi ambao hujishughulisha na kuuza vinywaji baridi, kushona nguo, kuchomelea vyuma na nyingine ambazo hutegemea umeme.

Tunaishauri TANESCO kutafuta majawabu kuhusiana na lipi lifanyike ili nchi yetu iondokane na adha ya kukatikakatika kwa nishati hiyo au mgawo kila uchao. Moja ya ufumbuzi wa tatizo hili ni kuanza kutumia teknolojia ya kufanya matengenezo ya umeme bila kuzima umeme.


Teknolojia hii imeshaanza kutumika katika nchi kadhaa barani Afriuka, na jambo la kujivunia ni kwamba Tanzania ina mtaalamu mzawa Mcdonald Liveline Technology LTD 123 Tanzania, ambaye katika miaka ya nyuma aliwahi kufanyakazi na TANESCO.

Mtaalamu huyo amekuwa akitoa mafunzo na kufanyakazi katika nchi kadhaa za Afrika kama Ghana, Zambia, Botswana na nyingine za kufanya matengenezo ya umeme kama kuhamisha nguzo, kukata miti bila kuzima umeme, hatua inayosababishia watumiaji na taifa kwa ujumla. Kwa nini tusiwaamini, kuwathamini na kuwatumia wataalamu wetu kama huyo badala ya kutumiwa na kuzinufaisha nchi zingine?

Tunaamini kwa kuwa serikali yetu ni sikivu, viongozi wakuu wa TANESCO na Wizara ya Nishati chini ya Waziri January Makamba, watauchukua ushauri wetu na kuufanyia kazi, ili kuwaondolea Watanzania kadhia ya kukatikakatika umeme na kuwaathiri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Operesheni 'safisha mji' imetakatisha barabara, kufufua fremu na masoko

Na Salome Mwasamale

**WASWAHILI** wanasema 'mnyonge mnyongeni haki yake mpeni'. Kwanini? Hivi karibuni tulishuhudia operesheni 'safisha mji' iliyowaondoa wafanyabiashara walioko pembezoni mwa barabara na walioweka biashara zao mbele ya maduka makubwa.

Hapo waliondolewa na kupelekwa katika masoko makubwa yaliyoandaliwa na serikali, kwa ajili yao. Ni operesheni iliyoleta usumbufu mkubwa kwa baadhi ya wafanyabiashara waliokuwa pembezoni, lakini ikarejesha neema kubwa kwa wenye fremu za maduka.

Tulishuhudia baadhi ya watu hata wasiokuwa wafanyabiashara wakilaumu operesheni hii, lakini baadhi yao walipongeza na kudai kuwa mji sasa unaonekana vizuri na utulivu upo, ikilinganishwa na awali walipokuwa barabarani, maana kulikuwapo msongamano mkubwa.

Operesheni sasa imeonyesha kuzaa matunda ambayo hata waliokuwa wanapinga, wanapongeza japo kimoyo moyo au kimyakimya.

Aina ya operesheni inatoa nafasi kwa fremu za biashara kwenye maeneo zilizokuwa hazitumiki, sasa zinagombewa na wafanyabiashara, tena kule ambako kulitelekezwa kabisa.

Pia, yanakuwa maeneo ambayo yanapandishwa bei sasa, pakiwekewa vitega uchumi vikubwa vinavyolipa ushuru na kuongeza pato la taifa.

Niende na mfano hai wa jijini Dar es Salaam niliko, jirani na Soko la Karume, ingawa ina ujumbe wa kitaifa, maana mustakabali wa mazingira na biashara tajwa yanafanana.

Mahali hapo tumeshuhudia maduka makubwa ya vitambaa yamejengwa na hata katika balaa hili la moto fremu hizo hazijaathirika kutokana na aina ya ujenzi imara wa kisasa.

Tunataka ujenzi wa masoko wa aina ile, ambao hata ikitokea hitilafu ya umeme au aina nyingine ya uhalifu kama kuacha mshumaa kama ule uliosababisha hasara kubwa katika Soko la Karume, hauachi vilio vikubwa na wala hausababishi madhara kwa jamii. Maeneo mbalimbali ya jiji hili sasa tunashuhudia ujenzi wa maduka makubwa na mazuri katika mpangilio bora, wafanyabiashara nao wanaonekana kuchangamkia fursa hizo, hata pato la taifa litaongezeka. Hivi sasa maeneo kwa mfano kama Chanika, Mvuti kwa Bwaja, Mwembeni. Msongola, Gongolamboto, Mbagala na mengine mengi yanapendezeshwa na maduka makubwa katika mpangilio bora, ambayo awali yalichafuliwa na vurugu za biashara ndogo nje ya maduka, taka zikatupwa hovyo, mitaro ikajazwa taka na kuziba.

Waache waseme wenyewe!...Mo Nurdin ni mfanyabiashara wa viazi eneo la Chanika, ambaye yuko wazi kumpongeza Rais Samia Hassan Suluhu, kwa kuwa na maono ya usafi wa jiji, kupitia kwa kuelekeza operesheni hiyo, inayoenda mbali kwa matokeo yake, ikitengeneza uhusiano mzuri kati ya wafanyabiashara na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Ni wazo linalomfikia hata Philipo Rali, mfanyabiashara wa nguo anayesema operesheni hiyo imepunguza ajali za barabarani na athari zake kwa wafanyabiashara walioko barabarani walioziba njia hata kukawapo msongamano.

Makamu Mwenyekiti wa Soko la Zingizilwa, Hassan Namkwacha, anaipongeza operesheni tajwa, akidai imesababisha kuboreshwa baadhi ya masoko yaliyokuwa tatizo kwa miaka mingi, hata kutelekezwa kabisa.

Anasema, Halmashauri ya jiji la Ilala sasa imeanza kuyafanyia marekebisho masoko mbalimbali yaliyopo katika jiji hilo, kwa kuyajengea mazingira rafiki kibiashara, ikiwamo miundombinu sokoni, akitoa mfano wa Zingizilwa, chumba kilichokuwa Shilingi 15,000 sasa Shilingi 30,000 kwa kuwa wafanyabiashara wameongezeka sokoni hapo.

Mkuu wa Masoko jijini Ilala, Victor Rugemalila, anasema pesa zimetengwa na jiji la Ilala kwa ajili ya kuwezesha uwezo wa kubeba watu 200 hadi 250 katika soko la Zingiziwa.

Rugemalila anasema mradi huo awamu ya kwanza utayagusa masoko ya Zingizilwa, Pugu Kajiungeni, Kigogo Freshi na Tabata Muslim.

Niseme asante Mama Samia kwa operesheni ,watu wameyakumbuka masoko yaliyosahaulika kwa muda mrefu.

HABARI KITAIFA

# Fedha UVIKO-19 zanufaisha wenye matatizo ya uoni hafifu

Na Salome Kitomari



SERIKALI imesema kuwa kupitia mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19, ilitenga Sh. milioni 704 kwa ajili ya kuchapa nakala 18,200 za wanafunzi wasioona.

Akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Khadija Taya, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga (pichani), alisema jana bungeni mjini Dodoma kuwa vitabu hivyo ni kwa ajili ya wanafunzi wasioona vya masomo yote ya sekondari.

Alisema nakala 9,100 ni vitabu vya nukta nundu na 9,100 ni vya michoro.

"Uchapaji wa vitabu hivyo upo katika hatua za mwisho na utakapokamilika vitasambazwa katika mikoa yote kulingana na mahitaji," alisema.

Naibu Waziri Kipanga alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika mikoa yote wakiwamo wanafunzi wasioona.

Akiuliza swali la nyongeza, Mbunge Taya alitaka kujua ni lini serikali itapeleka mwongozo kwa walimu wote kujua namna ya kufundisha wanafunzi wenye uoni hafifu kwa kuwa wanapata tabu kuona ubaoni na kusoma vitabu.

Alitaka kujua mkakati wa serikali kuongeza miundombinu ili wenye mahitaji maalum wasome vizuri na kuondokana vikwazo vilivyoko.

Akijibu maswali hayo, naibu waziri huyo alisema serikali inatambua uwapo wa dosari hizo na wizara iko mbioni kukamilisha mwongozo wa kushughulikia wenye uoni hafifu kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Under the Same Sun na utakapotiwa saini utasambazwa nchi nzima.

"Namhakikishia mbunge kuwa serikali imesambaza vitabu vya maandishi makubwa kwa wenye uoni hafifu kwenye shule za msingi na sekondari, mambo yanakwenda vizuri," alisema.

Kwa mujibu wa naibu waziri huyo, mgawanyo wa fedha za UVIKO-19 zilizotolewa ni Sh. bilioni 2.4 zimejenga matundu ya vyoo 2,200 na mchakato unaendelea kwa mengine 4,549 kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

# TRA yaanzisha kampeni kodi mlango kwa mlango

Na Salome Kitomari, DODOMA



SERIKALI kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imesema imeanzisha kampeni ya mlango kwa mlango ili kutatua kero zinazowakabili walipakodi.

Sambamba na kampeni hiyo, imesema inatoa elimu ya kodi, kuwatambua walipakodi wapya na kuwasajili kwa lengo la kurahisisha usajili wa walipakodi kwa kuwasogezea karibu huduma wafanyabiashara wote kwa kuwafuata katika maeneo yao ya biashara badala ya kuwasubiria waende TRA.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande (pichani), alisema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas.

Tarimba aliuliza ni kwa nini serikali isiiagize TRA kushuka mitaani ili kubaini biashara ndogo za maduka katika Manispaa ya Kinondoni kuzisajili na kutoa cheti cha kuidhinisha kuwa mfanyabishara hadaiwi (Tax Clearence) ili leseni zitolewe.

Mbunge huyo alisema utoaji wa leseni za biashara kwa biashara ndogo za maduka katika manispaa hiyo una changamoto nyingi kutokana na kukosa 'Tax Clearence'.

Alisema cheti hicho huwawezesha wafanyabiashara hao kusajiliwa na kupatiwa namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN Number).

"Katika kutatua changamoto hii kwa wafanyabiashara, serikali imeongeza kasi ya usajili wa walipakodi katika jiji la Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla," alisema Naibu Waziri.

Alisema kampeni hiyo ilianza Agosti, mwaka jana katika mikoa yote ya kikodi katika mkoa wa Dar es Salaam, ikiwamo Manispaa ya Kinondoni na itaendelea nchi nzima.

"Ni matumaini ya serikali kuwa suala hili litaongeza idadi ya walipakodi waliosajiliwa, hivyo kurahisisha upatikanaji wa 'Tax Clearance' ili leseni za biashara zitolewe kwa uharaka," alisema.

Pia Mbunge huyo katika swali la nyongeza alihoji kama serikali haioni umuhimu ikashuka chini kuandikisha wafanyabiashara kwa kuwa hajaiona hiyo kampeni huku akitaka serikali kuweka maofisa kodi ngazi ya kata na mtaa.

Alisema ni muhimu kuanzisha utaratibu wa kuwabaini wafanyabiashara wadogo kweye mitaa ili wapate elimu ya kodi ili utekelezaji uwe wa nadharia.

Naibu Waziri huyo alisema walipakodi 432,433 walisajiliwa kwenye kampeni hiyo kati ya hao 17,1973 ni wafanyabiashara.

Chande alisema serikali inashuka hadi serikali za mitaa kuwafikia wananchi, na kuhusu kuwa na maofisa wa kukusanya kodi ngazi za mitaa watalifanyia kazi

# Madiwani watakiwa ushirikishaji wananchi

Na Julieth Mkireri, RUFIJI

MKUU wa Wilaya ya Rufiji, Meja Edward Gowele, amewataka madiwani kufanya mkutano na kuelezea miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na serikali kutatua vikwazo mbalimbali kwenye jamii.

Meja Gowele aliyasema hayo juzi katika Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Rufiji ambapo alisema mikutano ni moja ya tiba kwa wananchi kwani inatumika kueleza yale yaliyotekelezwa na ambayo yanafanyiwa kazi.

Alisema madiwani ni moja ya viongozi wanaotegemewa kuisemea serikali kwa wananchi hivyo ni vema wakawaeleza wananchi kila kinachofanyika waelewe namna serikali yao inavyoshughulikia matatizo yao.

"Madiwani msibweteke kwa mafanikio yanayopatikana, nendeni mkafanye mikutano kuisemea serikali, mikutano ndio tiba inatoa fursa kwa wananchi kufahamu nini kimefanyika na wao kueleza kero zao ili zitatuliwe kwa wakati," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya pia amewataka madiwani kuhimiza wananchi kushiriki kwenye miradi ya maendeleo.

"Tumebaini kwenye miradi ya maendeleo wananchi hawashiriki ipasavyo, kuna baadhi tumetembelea kwenye miradi lakini hatujawakuta wananchi hii si nzuri," alisema.


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MOROGORO

MAOMBI NAMBA 57 YA 2021

AGNESS ALBIN AWETT na SAFARI SEBASTIAN
DHIDI YA
JUMA SAID MAGODI; MICHAEL CHIGOMA; JOHN MGANGA; AWADH MAKUSI; HALIMA KAZIULAYA; JOSEPH SONGALELI; ALEX STEPHAN MONJI; MICHAEL SAMSON; JUDITH D. MASHEGU; MICHAEL ARON; NEEMA MCHOME; ELIZABETH PIUS; ZAINA LUANDA; LUCY KEMBE; PIUS MSAGWA; FRANK FABIAN POLEA; MOHAMED ISSA; NEEMA KIHAGE; IDD ALPHONCE; ADAM LAGA; ISACK MELA; ABBAS SAID; BENJAMIN GEORGE; GABRIEL NYUNZA; ZIADA ALLY HUSSEIN; BASHIRU AMINI; ZABRON SUMBE; FAUSTI MAKOYE; MOHAMED ISSA MOHAMED; JONAS KOBOKO; DUES J. PETER; NARCIS M. LEENGA; LIGHTNESS ELIAKIM NDOWO; ALEX NYAMANDA; KISININI WILLIAM; HENERIKO ABEDI; EDGAR KAMUGISHA; ELIAS KAMUGISHA; ANTHONY NGATUNGA

WITO/KUITWA SHAURINI KWA:

Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 7/2/2022 mbele ya Mwenyekiti **E. Mogasa** nyinyi wenyewe binafsi au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 13 Mwezi January 2022

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

166889



IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)
AT DAR ES SALAAM
CIVIL CASE No. 77/2021
KUANG JIAN BIN……………………PLAINTIFF
VERSUS
KANAK INDUSTRIES DMCC…………………1ST DEFENDANT
FORTUNE CEMENT (T) CO. LTD………………2ND DEFENDANT
WENG TAK FUNG…………………………… 3RD DEFENDANT
PREM CHIMANLAL AHUJA……………………4TH DEFENDANT
NIHAR SURESH AHUJA…………………..........5TH DEFENDANT
MINAKSH PREM AHUJA……………………..........6TH DEFENDANT
SPANDAN PREM AHUJA……………..................7TH DEFENDANT
TO: WENG TAK FUNG,
COAST REGION.

SUMMONS FOR PUBLICATION.

Whereas the Plaintiff has instituted a suit against you, you are hereby summoned to appear in this court person or by a pleader duly instructed and able to answer all material question relating to the suit or who shall be accompanied by some person able to answer all such question on the 07th February, 2022 at 09:00 a.m. O'clock before Hon. Dr. J. L. Masabo J, to answer the suit, you must be prepared to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence. Take notice that, in default of your appearance on the day before mentioned, the appeal will be heard and determined in your absence given under my hand and the seal of this court this 6th day of January, 2022.

is court this 6th day of January 202

DEPUTY REGISTRAR
DAR ES SALAAM ZONE

166883

# Watembea kilomita 35 kufuata huduma za afya

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAGONJWA wakiwamo wajawazito katika kijiji cha Nyalwelwe, Ushetu wilayani Kahama wanatembea umbali wa zaidi ya kilomita 35 kwenda na kurudi kwa ajili ya kupata huduma za Kituo cha Afya cha Bulugwa.

Kilio hicho kilitolewa jana na baadhi ya wananchi wa kijiji hicho mbele ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga iliyotembelea na kukagua ujenzi wa majengo ya kituo cha afya katika eneo hilo.

Kituo hicho cha afya sasa kitakuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya wakazi 20,940 baada ya kukamilika.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyalwelwe, Alex Lukala, alisema wajawazito walikuwa wanateseka kutembea umbali mrefu wanapopewa rufani ya kwenda kituo cha afya kupata matibabu.

Pia alisema wananchi hao pia hawakuwa na huduma ya chumba cha kuhifadhia maiti wanapofiwa.

Diwani wa kata ya hiyo, Kulwa Emanuel, alisema kulikuwa na msongamano wa wagonjwa kutoka vijiji 11 vya jirani vinavyowazunguka ambavyo vina wakazi zaidi ya 57,000.

Alisema kwa kipindi kirefu hawakuwa na huduma za upasuaji pamoja na kulaza wagonjwa ambao walikuwa wakifikishwa hapo.

Kwa sasa, alisema shida mbalimbali zimeanza kutatuliwa baada ya kupandisha hadhi zahanati yao na kuwa kituo cha afya ambacho kimefikia hatua nzuri katika ujenzi wake.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati hiyo, Dk. Mafwele Kasomelo, alisema walipokea Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa majengo.

"Kituo hiki kimeelemewa na idadi kubwa ya watu wanaotaka huduma wakiwamo wajawazito 1,920 hadi 2,160 kwa mwaka, watoto wa umri chini ya miaka mitano 4,271 na wagonjwa wa nje 8,400," alisema Dk. Mafwele.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) ya CCM, Gasper Kileo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fedha za kujenga kituo hicho cha afya.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema shida mbalimbali za wananchi zitatatuliwa na serikali kwa kupeleka fedha za miradi mbalimbali.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Judith Nguli, akishiriki ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Barikiwa, alipokwenda kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho, juzi. Anayeshuhudia ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Mohamed Kitura. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yahimiza upandaji miti

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KATIBU wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Morogoro Mjini, Hussein Egobani, amewashauri vijana kujikita katika kuboresha mazingira kwa kupanda miti.

Amesema miti ni uhai, maji na ajira itakayowaingizia vijana kipato badala ya kukaa vijiweni wakipoteza muda.

Egobani aliyasema hayo jana alipozungumza na vijana kutoka UVCCM Wilaya ya Morogoro Mjini walipokuwa eneo la Bwawa la Mindu wakipanda zaidi ya miche 3,000 kati ya 25,000 inayokusudiwa kupandwa kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka 45 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Februali 5 mwaka huu.

Egobani alisema UVCCM inatarajia kupanda miti 5,000 hadi 25,000 katika eneo linalozunguka Bwawa la Mindu ili kulinda chanzo hicho cha maji.

Kamanda wa Kikosi na Shirika la Mzinga Morogoro, Meja Elihuruma Mnyenye, aliwasisitiza wakazi wa Manispaa ya Morogoro kushirikiana kwa karibu katika kupanda miti kuzunguka eneo la Bwawa la Mindu na kufanya kuwa msitu ili jeshi lilinde vyema kama lilivyopewa jukumu.

Meja Mnyenye alisema wamepewa jukumu la kulinda bwawa hilo ambalo linatumiwa na karibu asilimia 80 ya wakazi wa Manispaa ya Morogoro.

Meneja Biashara kutoka Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mkoa wa Morogoro (MORUWASA), Lyang'ong'o Kiguhe, alisema ili kulilinda bwawa hilo, MORUWASA ina lengo la kupanda miti zaidi ya 500,000 mwaka huu.

Kiguhe alisema bwawa hilo linalopokea maji kutoka mito mitano ya Mzinga, Lukurunge, Mgera, Mlali na Ngerengere, likizungukwa na miti ipasavyo, litakuwa katika ulinzi unaoleta faida za kijamii na hata kiuchumi, akiiomba UVCCM kuendelea kuwaunga mkono katika shughuli za utunzaji mazingira na kufanikisha upandaji miti kwenye eneo hilo.

Alisema kampeni ya upandaji wa miti ndani ya mita 60 kutoka kwenye kingo za mito na ndani ya mita 500 husaidia utunzaji wa mazingira na kuwapo ubora wa maji yanayotumika ambayo yanaweza kuonekana sio safi kama watu watafanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 au ndani ya mita 500 kutoka kwenye vyanzo vya maji.

Katibu Hamasa UVCCM Kata ya Mkundi, Rukia Ramadhani, alisema vijana wameamua kujitokeza kupanda miti ili kuimarisha mazingira ya bwawa hilo ili yawe salama kwa manufaa ya wakazi wa Manispaa ya Morogoro.

# TEMESA yatakiwa kujitathmini utendaji

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Balozi Aisha Amour, ameitaka Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), kujipanga upya ili kukidhi matarajio ya taasisi hiyo kwa serikali.

Akizungumza jana baada ya kukutana na menejimenti na mameneja wa TEMESA wa mikoa, Balozi Amour aliwataka watendaji hao kuleta mabadiliko makubwa ya utendaji, hivyo kuvutia taasisi za serikali na wadau wote kutumia huduma za wakala.

"Kila mtumishi awajibike kikamilifu kuanzia leo (jana). Boresheni huduma zenu na mwangalie upya gharama za utengenezaji wa magari ili kuwavuta wateja wengi kutumia huduma zenu," alisema Balozi Amour.

Pia aliitaka TEMESA kutathmini upya gharama zake katika utengenezaji wa magari na kuhakikisha inaboresha kitengo cha huduma kwa wateja.

Kuhusu vivuko, aliwataka mameneja wanaosimamia vivuko nchini kuhakikisha vinatoa huduma bora na kwa wakati ili kuepuka udanganyifu katika ukusanyaji wa mapato.

"Simamieni uadilifu wa watumishi wenu kwa kufuata taratibu, kanuni na miongozo katika mazingira yenu ya kazi", alisisitiza Balozi Amour.

Pia aliwataka watendaji wote wa taasisi zilizo chini ya sekta ya ujenzi kuthibiti utoro na kuhakikisha watumishi wanapata stahiki zao kwa wakati ili kuwajengea motisha ya kufanya kazi kwa bidii.

Naye Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kilahala, amemhakikishia Katibu Mkuu kuwa TEMESA imeandaa mkakati wa mabadiliko utakaotekelezwa hivi karibuni ili kupunguza changamoto na malalamiko mengi kwa watumiaji wa huduma za wakala.

Alisema mkakati huo pia utawezesha wataalamu wa TEMESA kupata mafunzo ya mara kwa mara ili kuwawezesha kumudu kutengeneza magari ya kisasa yanayotengenezwa kwa teknolojia ya hali ya juu.

Katibu Mkuu Balozi Aisha Amour yuko katika ziara ya kukagua miradi na kukutana na watendaji wa taasisi zilizo chini ya sekta ya ujenzi na ameambatana na Naibu Katibu Mkuu, Ludovick Nduhiye.

## HABARI KITAIFA

## Wanufaika TASAF wabainisha sababu kujitosa ufugaji

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa**
HANDENI

WALENGWA wa mpango wa kunusuru kaya maskini, unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wameelezea namna walivyoingia kwenye ufugaji kwa ajili ya kujiongezea kipato.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wilayani Handeni, walisema chanzo cha kuanza ufugaji huo kilitokana na kuwekeza kidogo pesa waliyokuwa wakipatiwa na TASAF.

"Nilianza na mbuzi mmoja kufuga na huyo nilimnunua kwa Sh. 35,000 baada ya kujibana kifedha kidogo ninayopewa na TASAF, na hiyo ni baada ya kutoa ya matumizi yote muhimu ikiwamo ya chakula na mengine ya wanafunzi," alisema Fatma Ramadhani mnufaika kutoka Mkata Mashariki.

Fatma alisema aliendelea na utaratibu huo wa kuongeza mifugo kwa kuwekeza kidogo kidogo kila pesa aliyokuwa akipata na mpaka sasa ana mbuzi zaidi ya 20.

"Na malengo yangu ni kuongeza mbuzi zaidi ya hawa, ninaamini kwamba kupitia mifugo nitajiongezea kipato zaidi na nitafika mbali kimaendeleo na kuondokana na shida ndogo ndogo,"alisema Fatma. Fatma Muya, mlengwa wa TASAF ambaye pamoja na shughuli nyinginezo, yeye anafuga ng`ombe na kuku ambao alisema aliwapata baada ya kuingizwa katika mpango huo wa kunusuru kaya maskini.

"Kupitia TASAF, nimenufaika na mambo mengi sana, nimetoka katika maisha ya kutaabika niliyokuwa nayo mwanzo kabla ya kuingia na sasa niko vizuri. Wakati naanza kupokea pesa nilianza kuwekeza kidogo na nikawa nafanya biashara ndogo ndogo," alisema Muya.

"Mpaka sasa kati ya vitu nilivyo navyo ambavyo nimenufaika ni pamoja na ng`ombe wa maziwa wawili, naishukuru sana TASAF kwa kunifikisha hapa nilipo."

Mbali na ng`ombe, pia alisema anafuga kuku na kwamba mpaka sasa wako 15.

"Na hawa kuku wakati mwingine nikipata shida ya haraka ndio huwa natumia kuuza na naendelea kupambana kuwalisha vizuri ili waendelee kuzaliana," alisema Muya.

# RC ataka wazawa wanufaike na mgodi

**Na Faustine Feliciane,**
KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amesema Watanzania hususani wenyeji wa Mkoa wa Shinyanga wanapaswa kunufaika na uwapo wa Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu kwa kupewa nafasi ya kufanya biashara kwa kuuza malighafi zinazohitajika mgodini huko.

Akizungumza wilayani hapa, Mjema alisema zipo malighafi zinazohitajika kila siku mgodini, hivyo ni vyema wazawa kupewa fursa ya kuuza na kufanya biashara na mgodi huo.

"Huu mgodi ni wa Watanzania kwa sababu kuna muungano wa kampuni zinazoendesha mgodi huu. Kuna Barrick na Twiga ambayo ni kampuni ya Kitanzania, lakini yapo mahitaji mbalimbali yanayohitajika mgodini, Watanzania lazima wanufaike kwa kuuza malighafi hizo na kufanya biashara," aliagiza. Alisema mgodi huo wa Bulyanhulu utaendelea kuwapo mpaka mwaka 2045, hivyo ni vyema kipindi hicho chote Watanzania waendelee kunufaika.

Kuhusu masuala ya kimaendeleo kwa jamii yanayofanywa na mgodi huo, Mjema alisema kwa sasa uongozi wa mkoa umeamua kuwashirikisha wabunge na viongozi wengine kwenye kamati za maendeleo za vijiji vinavyozunguka mgodi huo (CDC) ili kuhakikisha mgodi huo unanufaisha mkoa mzima.

"Wabunge nao watapata fursa ya kuchangia mawazo na mipango ya maendeleo kabla ya kuwapelekea wenzetu wa mgodi kwa utekelezaji, na jambo zuri ni kwamba wenzetu hawa wapo tayari kufanya kile ambacho tutapanga," alisema.

Mjema alisema walikubaliana wananchi wenyewe ndiyo waamue ni maeneo gani wanataka kusaidiwa na Barrick.

"Tutakuwa tukifanya tathmini ya pamoja juu ya maeneo ambayo tunaona tunahitaji msaada, wananchi wenyewe kwenye vikao vya kamati ya maendeleo watakuwa wakiainisha maeneo ambayo wanataka kupatiwa msaada na baadaye tunawapelekea wenzetu wa Barrick kwa ajili ya kuchukua hatua. Sasa hivi wenzetu wa Barrick ndiyo wanapanga wafanye nini," alisema.

Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow, alisema mgodi huo unashirikisha wadau wengine wazawa katika mambo mbalimbali. Alisema wanatumia pia malighafi nyingine za ndani ya Tanzania pamoja na kuingia mikataba na kampuni zingine za Kitanzania kwenye miradi mbalimbali ndani ya migodi ya Barrick.

"Kwenye suala la maendeleo tunaendelea kushirikiana na wananchi wanaozunguka migodi yetu na tupo tayari kutekeleza miradi mbalimbali tutakayokubaliana kama ambavyo tumekuwa tukifanya hivyo kwenye sekta za afya, maji na elimu," alisema Bristow.

Aliongeza kuwa wanaendelea kushirikiana na serikali na uongozi wa Mkoa wa Shinyanga katika kuhakikisha wanasaidia jamii inayowazunguka.



Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia (kushoto), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi wa African Child Project, Catherine Kimambo, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ya kuendesha sekta ya elimu kwa njia ya mtandao kupitia mpango wa 'School Connectivity Project', utakaosaidia kuongeza ufaulu kwa asilimia tano kwa wanafunzi nchini. Katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Mhandisi Samson Mwela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau waombwa udhibiti ukatili kijinsia

**Na Sabato Kasika**

KAMATI ya Mkakati wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Mkoa wa Dar es Salaam, imewaomba wadau kuendelea kushirikiana nayo, ili kufanikisha vita dhidi ya vitendo vya udhalilishaji, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika jamii.

Ombi hilo lilitolewa jana na mwenyekiti wa kamati hiyo, ambaye pia ni Mganga Mkuu wa mkoa huo, Dk. Rashid Mfaume, kwenye mkutano wa kutambulisha mradi wa majaribio unaolenga kuzuia, kukabiliana na udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono.

Utambulisho huo ulifanywa na Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Wakili Anna Henga, ambaye alielezea jinsia unavyofanyika wilayani Kinondoni na mafanikio yake.

"Kwanza kabisa niwapongeze LHRC kwa kazi nzuri mnayofanya, kwani vitendo vya ukatili huo vipo ndani ya jamii kuanzia katika familia, hivyo ni vyema kila kiongozi kwenye eneo lake hata wajumbe wa nyumba kumi kufuatilia na kutoa taarifa," alisema Dk. Mfaume.

Aliongeza; "Pamoja nayo, tunawaomba wadau mkiwamo nyie LHRC. Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) na wengine kuendelea kushirikiana na MTAKUWWA hata kwa kutoa rasilimali zenu ili kufanikisha vita hii katika jamii." Mganga Mkuu huyo alisema, Dar es Salaam ni mkoa wenye watu wengi na kufafanua kuwa, uwezekano wa kuwapo vitendo vingi vya ukatili ni mkubwa na kwamba jambo la msingi ni ushirikiano wa wadau wote ili kuvikomesha.

Akielezea kuhusu mradi huo, Mkurugenzi wa LHRC alisema, utafiti uliofanywa na kituo hicho mwaka 2019/202, ilibainika kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kingono katika Wilaya ya Kinondoni.

"Kuna matukio takribani 57,626 na kati ya hayo mengi yalikuwa udhalilishaji na ukatili wa kijinsia hasa udhalilishaji wa kingono. Kutokana na hali hiyo, kituo kiliingia makubaliano na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kutekeleza mradi wa majaribio," alisema Henga.

Alisema lengo lilikuwa ni kujenga uwezo na kuhamasisha wadau mbalimbali, ili kuzuia na kukabiliana na changamoto za matukio ya udhalilishaji wa kingono kwa makundi mbalimbali na kufanya tathmini ya jinsi ya kuandaa programu za kukabiliana na vitendo hivyo kuwa zenye tija na ufanisi.

"Mradi huu unatekelezwa katika Hospitali ya Mwananyamala ambayo ni Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dar es Salaam na jamii inayoizunguka zikiwamo Kata za Mwananyamala na Makumbusho," alisema.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa mradi huo wa kipindi cha miezi takribani mitatu, unatekelezwa kwa pamoja na wadau wengine wakiwamo madiwani, wenyeviti na watendaji wa serikali za mitaa na kata katika eneo la mradi.

"Kuna Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto, maofisa wa elimu, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii ngazi ya mkoa, manispaa na kata, wanafunzi na walimu wa shule za sekondari na msingi katika eneo la mradi," alisema. Aliwataja wadau wengine kuwa ni klabu za michezo, madereva wa bodaboda; wanahabari, asasi za kiraia na wadau wengine wenye nia moja na malengo ya mradi.

"Mapambano dhidi ya tatizo gumu la unyanyasaji wa kingono na kijinsia yanahitaji ushirikiano na jitihada za pamoja kati ya jamii, sekta, asasi na taaluma mbalimbali," alisema.

Henga alisema, kwa ushirikiano huo, mradi huo umekuwa na mafanikio ikiwamo kupokelewa vizuri na wadau wote, kwa kushiriki tangu hatua ya awali, na kwamba unaweza kuibadilisha jamii ikaacha na ukatili.

# Serikali yasema suluhisho ni kujua visababishi afya akili

SERIKALI imesema kuna haja ya kushughulikia visababishi vya ongezeko la wagonjwa wa akili nchini, badala ya kujenga hospitali nyingine kama ilivyoshauriwa na baadhi ya wabunge.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi, aliyetaka kujua mpango wa serikali kujenga hospitali nyingine mbali na Mirembe, mkoani Dodoma.

Alisema kwa sasa kuna ongezeko la wagonjwa wa afya ya akili hususan vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35 kwa sababu mbalimbali za maisha na kwamba kuwapo kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itashughulikia kwa karibu visababishi hivyo.

"Tunapaswa kuangalia visababishi na si kujenga hospitali nyingine. Tumeanza na Kigoma ambako walipewa bajeti ya kutosha ili wapate tiba. Kwa sasa tunapiga CT- Scan za ubongo ili watibiwe, lakini lazima tushughulikie visababishi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mollel, katika kusogeza huduma kwa wagonjwa wa afya ya akili, serikali ina mkakati wa kujumuisha huduma hizo kwenye hospitali zingine zilizojengwa.

Pia alisema Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Temeke iko katika mchakato wa kukarabati jengo lililokuwa linatumika kwa wagonjwa wa kisukari kulaza wagonjwa wa akili.

Dk. Mollel alikuwa akijibu swali la msingi la Mbunge Kisangi aliyetaka kufahamu mpango wa serikali wa kujenga wodi za wagonjwa wenye matatizo ya ubongo na akili katika hospitali za rufani za katika mkoa wa Dar es Salaam za Temeke, Amana na Mwananyamala.

Alisema Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala imetenga Sh. milioni 200 kwenye bajeti ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya wagonjwa wa akili.

"Pia Hospitali ya Rufani ya Amana kwa kuwa ujenzi huu uko kwenye mpango mkakati wa miaka mitano, wameelekezwa kutenga bajeti ya ujenzi wa jengo la afya ya akili katika bajeti ya mwaka 2022/23," alisema.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, akijibu baadhi ya maswali yaliyoulizwa na wabunge, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Fedha za BADEA kukarabati stendi ya Musoma

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imeandaa andiko la kuboresha stendi ya mabasi ya Bweri ili kuondoa kero iliyoko sasa.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ghati Chomete, aliyetaka kujua ni lini ahadi ya Rais kuhusu ujenzi wa stendi hiyo utakamilika.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema fedha hizo zitatokana na ufadhili wa Benki ya BADEA.

"Tayari Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imeandaa andiko la mradi huo na limeshawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi wa kutengewa fedha kutekeleza ujenzi wa mradi huo kupitia ufadhili wa Benki ya BADEA," alisema.

"Serikali inaendelea na taratibu za kupata ufadhili huo ili mradi huo pamoja na miradi mingine inayotarajiwa kutekelezwa kupitia ufadhili huo utekelezaji wake uweze kuanza," aliongeza Naibu Waziri. Alisema stendi ya mabasi ya Bweri ilijengwa mwaka 2007 kwa mapato ya ndani ya halmashauri kwa kutumia mkandarasi CMG Construction Company Limited aliyeingia mkataba wa Sh. bilioni 1.36 na kwamba alifanya kazi zenye thamani ya Sh. milioni 921.17.

Naibu Waziri alisema kwa sasa stendi hiyo yenye uwezo wa kuingiza magari 35 hadi 45 ina miundombinu iliyochakaa hivyo inahitaji kuboreshwa.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo akijibu swali la Mbunge wa Manonga (CCM), Seif Gulamali, alisema serikali inaendelea kujenga vituo vya kutolea huduma za afya katika mamlaka za serikali za mitaa ili kuboresha utolewaji wa huduma ya afya ya msingi kwa wananchi.

Mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itatekeleza ahadi ya Rais kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ziba wilayani Igunga, aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi 2020.

"Ujenzi na ukarabati wa vituo unahusisha utekelezaji wa ahadi za viongozi kwa kadri ya fedha zinavyopatikana. Katika kutekeleza mkakati huu, serikali imepeleka Sh. bilioni 58.25 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vipya vya afya 207 katika tarafa ambazo zilikuwa hazina vituo vya afya na kata 26 za kimkakati,"alisema.

Pia alisema serikali imepeleka Sh. milioni 250 katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika kata ya Ziba na kwamba wataendelea kutekeleza ahadi za viongozi kujenga au kukarabati vituo hivyo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

## Viwanja vinne vya ndege kujengwa, kukarabatiwa

SERIKALI imesema miradi minne ya ujenzi na kukarabati viwanja vya ndege kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na kwamba makandarasi wameshapatikana na kazi itaanza karibuni.

Hayo yalisemwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, huku akivitaja viwanja hivyo kuwa ni Kigoma, Tabora, Sumbawanga na Shinyanga.

Alisema hayo wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Buhigwe (CCM), Kavajuru Felix, aliyetaka kujua mkakati wa serikali kupanua uwanja wa Kigoma ili ndege kubwa zitue.

Naibu Waziri alisema miradi hiyo imeshapata makandarasi isipokuwa kiwanja cha ndege cha Kigoma.

"Kwa sasa taratibu za makubaliano ya kimkataba tayari zimekamilika kati ya serikali na mfadhili (EIB)," alisema.

Alisema pamoja na mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kuwa na mfadhili EIB, kazi zingine ambazo ziko nje ya makubaliano zitatekelezwa na serikali moja kwa moja.

Aidha, alisema serikali itahusika na kazi ya urefushaji wa barabara ya kuruka na kutua ndege kutoka mita 1,800 hadi 3,100 na kwamba tayari usanifu wa kina umefanyika kwa lengo la kuwezesha ndege kubwa kutua na kuruka bila matatizo yoyote.

Pia alisema serikali inasubiri idhini kutoka kwa mfadhili ili kukamilisha mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi atakayetekeleza mradi huu.

Alizitaja kazi ambazo zinatarajiwa kufanywa kwa ufadhili wa benki hiyo ni ujenzi wa jengo jipya la abiria, jengo la kuongozea ndege, upanuzi wa maegesho ya ndege, usimikaji wa taa za kuongozea ndege pamoja na uzio wa usalama.

"Serikali imejipanga kuanza upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma mara baada ya kumpata mkandarasi atakayetekeleza mradi huu," alisema.




Habari zote na Augusta Njoji na Salome Kitomari

ama
ALHAMISI FEBRUARI 3, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**MAGONJWA YASIYOPEWA KIPAUMBELE...**
**Trakoma: Maradhi yanayotisha hatima ya wengi kumudu kuona**



Ukurasa 12

**Fahamu namna unyanyasaji unavyodhuru afya ya mtoto kimwili, hadi kisaikolojia**

# Usalama wake mtoto ulikojikita na kingo za sheria zinazomtetea

**Na Honesta Kaaya, SJMC**

JAMII kwa maana ya binadamu katika nafasi zake wamegawanyika katika nafsi kadhaa, kuu ni kijinsia kwa maana ya wanaume na wanawake, pili umri.

Hapo napo watu wanagawanyika katika maeneo kadhaa; wazee, watu wazima, wa kati, vijana na watoto, ambao kwa tafsiri ya sheria inayowahusu nchini ni umma wenye umri chini ya miaka 18.

Mapatano ya kimataifa kuhusu Haki za Watoto yamekubaliwa na wanachama wa Umoja wa Mataifa, ndio yanazaa tafsiri ya mtoto iliyopo nchini katika Sheria ya Watoto 2009.



Watoto wakiwa mchezoni. **PICHA: MTANDAO.**

**ASEMAVYO MWANASAIKOLOJIA**

Mwanasaikolojia katika Hospitali ya Manispaa ya Ubungo, Dk. Hashim Limila (inayoendelea kujengwa), anafafanua haki za watoto zinajumuisha kushirikiana na wazazi wote wawili, kutambuliwa kibinadamu na mahitaji ya msingi ya ulinzi wa mwili.

Pia, anataja haki ya chakula, huduma za afya na sheria zinazofaa kwa ukuaji mtoto, haki za kiraia, uhuru na kutobaguliwa kwa rangi, jinsia, asili, ulemavu, dini na kabila.

Anafafanua namna inavyowapa watoto tafsiri ya haki zinazolenga kuwajengea uhuru kimwili, kiakili na kimhemko kutokana na unyanyasaji.

Wakati watoto wote wanatajwa kuwa na haki ya kulindwa na kuishi salama chini ya ama wazazi au walezi ambao nao wanatambuliwa na kutafsiriwa hadhi katika Sheria ya Watoto, 2009 kwa matarajio wakue katika mazingira salama.

Familia ndicho chanzo cha ulinzi wa mtoto, wazazi au walezi wengine wana jukumu la msingi la kutengeneza mazingira ya nyumbani ambayo ni salama na yenye upendo.

"Pia, shule na jamii ina jukumu la kutengeneza mazingira ya nje ya nyumbani ambayo ni salama na rafiki kwa mtoto,"anafafanua mwanasaikolojia huyo.

Ukweli uliopo, ikiwamo taarifa zinazosambaa kupitia nyanja mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari, zinaonyesha kuwapo kundi kubwa la watoto wanaokosa ulinzi na usalama unaotakiwa

Aina hii ya ukiukwaji haki za watoto inapunguza uwezekano wao wa kuishi, kukua vizuri na kufikia ndoto zao. Ni vyema, wasichana na wavulana wakahimizwa na wasaidiwe ili wazungumze kuhusu utetezi wa haki zao kama watoto," anafafanua.

Anaendelea: "Vijana hawana budi kuwa msitari wa mbele katika ulinzi wao wenyewe dhidi ya unyanyasaji na ukatili."

Sheria ya Mtoto ya 2009 ina ufafanuzi kwamba kila mtoto ana haki ya kukulia katika familia na endapo familia haina uwezo wa kumhudumia mtoto, mamlaka katika jamii husika zichukue hatua ya kujua sababu za hali hiyo, huku mbadala wa malezi na matunzo ya mtoto yakifanyika.

Sheria hiyo inaelekeza haki ya kwanza ya motto ni kuishi na wazazi wake au mbadala wa walezi na asiwapo wa kuzuia haki hizo, familia ikiratibu maandalizi ya mtoto kuwa na mazingira salama ya kuishi na makuzi, isipokuwa ikiamuliwa vinginevyo na mahakama, kwa maslahi ya usalama wa mtoto.

" Mtoto atakuwa na haki ya jina, utaifa nakuwafahamu wazazi wake wa kumzaa na ndugu wengineo.

"Watoto wadogo wa jinsi zote yaani wakike na wakiume hawana budi kulindwa dhidi ya aina zote za ukatili na unyanyasaji,"inaeleza sheria, ikitafsiri unyanyasaji unagusa kimwili, kingono na kihisia.

Wasichana na wavulana wanaweza kufanyiwa ukatili na unyanyasaji wa kingono katika maeneo ya nyumbani, shuleni, kazini au ndani ya jamii.

"Ni lazima hatua zichukuliwe kuzuia hali hiyo, pia kwa watoto ambao wamefanyiwa vitendo vya unyanyasaji na unyonyaji wa kingono wanaohitaji msaada wa haraka wa kuwawezesha kuondokana na hali hiyo," anafafanua mwanasaikolojia Dk. Limila.

**KUTOKA WORLD VISION**

Asasi ya World Vision nchini inaorodhesha haki za mtoto katika maeneo makuu manne kwa maana ya: Kuishi, inayogusa kumlinda na kuendeleza uhai wa mtoto, ikiwamo umuhimu wa lishe na tiba bora, mavazi, maji na usafi .

Pili, anataja haki ya kuendelezwa kiakili, kwa maana ya elimu rasmi na isiyo rasmi, kiroho, mila na desturi.

Tatu, ni mtoto anapaswa kulindwa dhidi ya unyanyaswaji, ubaguzi, ukatili wa kimwili, kingono na kihisia, kunyonywaji kwa namna zote, ikiwamo kudhibiti ajira za utotoni.

Pia, haki ya mwisho ni ya kushiriki kutoa maoni wakitakiwa kuwa na haki za kidemokrasia wakitoa mawazo yanayozingatiwa kwa uamuzi wa yanayo athiri maisha yao.

AFYA

# Fahamu namna unyanyasaji unavyodhuru afya ya mtoto kimwili, hadi kisaikolojia

## •Simulizi za wataalamu na mikasa ya Mara

**Na Igembya James, SJMC**

UNYANYASAJI, uonevu na ukatili dhidi ya watoto ni suala linalokuwa kwa kasi duniani, wengi wakitendewa mambo yasiyoendana na malezi yao kiumri na kiafya.

Hiyo tafsiri yake inaangukia katika uvunjaji sheria na haki za mtoto, kwa kushuhudiwa athari za kimwili, kimaadili au kihisia, ikiwamo vipigo, kutukanwa, kubaguliwa, kutojaliwa unyanyasaji wa kingono na utumikishwaji.

Haki za mtoto zimeainishwa moja kwa moja katika Sheria ya Mtoto Tanzania ya Mwaka 2009, ikimtaja ni mwenye umri chini ya miaka 18 na atakuwa na haki kuishi huru bila ya ubaguzi wa aina yeyote, kwa maana ya jina, utaifa au kufahamu wazazi na ndugu wengine kifamilia.

Hiyo inatajwa kuwa ni sambamba na kuishi na wazazi au walezi, isipokuwa tu kama kuishi na wazazi au familia kutaleta madhara kwa mtoto awe katika hatari ya unyanyasaji na hakuna manufaa kwake.

Kumekuwapo mikasa mingi ikiripotiwa kwa mamlaka husika dhidi ya unyanyasaji, uonevu na ukatili kwa watoto ambazo baadhi zimeacha simanzi na maumivu kwa ndugu, jamaa na walio karibu na mwathirika.

Hapo panatajwa mikasa kama ya vifo, ulemavu na magonjwa yatokanayo na ama unyanyasaji au uonevu kwa mtoto.

Kwa kurejea ripoti ya Polisi nchini iliyonukuliwa na redio ya kigeni Aprili mwaka huu, kuna ongezeko la asilimia 25.95 la ukatili dhidi ya watoto katika mwaka 2020, mikasa 7388 iliyoripotiwa kitaifa, tofauti na mwaka 2015 kulikuwapo matukio 5,803.

Watetezi wa haki za watoto wanataja imani za kishirikina na utandawazi ni miongoni mwa sababu za ongezeko la matukio hayo.

Ni taarifa zinazochukua nafasi, huku ikitangazwa kwamba ni kipindi ambacho wazazi na walezi wengi wanatajwa kutokuwa karibu na watoto wao, wengi wakihangaikia mahitaji ya msingi ya watoto.

**KILIO VS UKEKETAJI**

Mkoani Mara ndiko kunatajawa kuwapo mikasa mingi ya unyanyasaji na ukatili kwa watoto, hasa ukeketaji. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) nacho kinasema ukeketaji mabinti umekithiri mwaka 2020, ikiwa imejikita ndani ya mila na desturi za wenyeji.

Sura mojawapo ni kuongezeka idadi ya wasichana wanaokimbia familia zao kutafuta hifadhi kwingineko, ikiwamo katika nyumba salama zilizoanzishwa na wadau wanaopinga ukatili huo kwenye mkoa husika.



Kikao kinachohusu udhibiti wa ukeketaji kikiendelea.

**MKASA ULIVYO**

Mkasa mmojawapo unamhusu msichana mmoja (jina tunalo) mwenye umri wa miaka16 wilaya ya Butiama mkoani Mara, aliyekeketwa baada ya kushindwa kujiokoa dhidi ya ukeketaji husika.

Inaelezwa kwamba, baada ya kukeketwa aliweza kukimbia kukwepa hatari iliyofuata kuolewa katika umri huo mdogo. Anafafanua: "Baba alinilazimisha mimi na dada yangu tukeketwe akasema kwamba tusipokeketwa atatuua. Akatukeketa!

"Alipotukeketa, akampeleka dada yangu shule akaniacha mimi, akaniambia kwamba 'wewe nataka unipe mahari'...Mwaka 2019 wachumba wakaanza kuja, akanichagulia mume akasema, 'sasa nataka uolewe ili nipate mahari'.

"Nikasema baba mimi sitaki mimi ni mdogo, akasema kwamba 'sitaki kusikia upuuzi wako na utaolewa kwa lazima ng'ombe 11 hizo siwezi kuziacha...' "Nikatoroka nyumbani nikalala na kushinda njaa siku mbili, Mama Kurwa alikuja usiku saa 10 akanileta shirika la Hope,"

**WADAU WANAVYONENA**

Wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, Shirika la Hope for Girls and Women in Tanzania (HGWT), pamoja na Association for Termination of Female Genital Mutilation (ATFGM), kwa kushirikiana na serikali wameanzisha nyumba salama tatu wilayani Serengeti, Butiama na Tarime, mahsusi kusaidia wasichana waliokimbia familia zao wakihofia ukeketaji.

Pia, kuna mtandao wa kisiasa ambao Aprili mwaka juzi, umetaja vita dhidi ya ukeketaji mkoa wa Mara yazidi kuota mizizi, ikirejewa simulizi yao msichana mwenye umri wa miaka 14 mkazi wa wilayani Serengeti, kukeketwa saa saba za usiku hata kukamsababishia kuvuja damu nyingi na akazimia kwa saa kadhaa.

Huyo ni mwanafunzi wa darasa la sita mwenye ndoto ya kuwa daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake, sasa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Nyerere.

**KUTOKA KWA WATAALAMU**

Mganga Mkuu Mfawidhi, Dk. Tanu Waryoba, anathibitisha kumpokea msichana huyo, huku Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shillah, akikemea vikali tukio hilo la binti kukeketwa.

Kutoka mtandao wa Wildlaf February 24 mwaka juzi, inaelezwa ukatili tajwa una matokeo mabaya kwa wanawake na watoto, sambamba na madhara ya kudumu maishani na yanayoweza kuharibu fursa ya mtu kuishi vizuri kiafya na penye mafanikio.

Inatajwa, ukatili dhidi ya wanawake na watoto una athari kiafya, kimwili, kisaikolojia na kiroho, ukiathiri uwezo wa mwanamke kushiriki masuala ya kiuchumi hata kufifisha uwezo katika uboreshaji maisha ya familia.

Lingine katika mustakabali huo wa kitaalamu ni kwamba, ukuaji ubongo unaathirika pindi wanapopatwa au kushuhudia vitendo vya kikatili.

Pia, ukuaji mwili na afya nao unaathirika kuishia mtoto kushindwa kufanya vizuri masomoni anakuwa na tabia isiyokubalika katika jamii na shuleni.

Nicolaus Magesa, mtaalamu wa mambo ya afya, anayepatikana katika Hospitali ya Rufani Mbeya, anaeleza: "Mtoto mwenye umri wa miaka sifuri hadi minane, anaweza kupata utapiamlo pale anapopitia manyanyaso kama vile kunyimwa chakula na kuanzia miaka nane hadi kumi na nane."

Anaendelea: "Kuna uwezekano mkubwa wa kupata msongo wa mawazo unaweza kupelekea magonjwa mbalimbali kama vile magonjwa ya akili.

"Kubwa, ni maumivu na majeraha yanayoweza pelekea kifo kwa mtoto inategemeana na aina ya unyanyasaji na uonevu kwa mtoto."

Mtaalamu wa afya, Matiku Makoye ana maoni: "Unyanyasaji wa kutopata huduma za afya kama kukosa chanjo kunaweza kusababisha kupata magonjwa ya kudumu, magonjwa hatarishi, unyanyasaji kwa watoto hasa kipigo kinaweza sababisha ulemavu wa kudumu."

Pia, anafafanua kwamba: "Unyanyasaji wa kingono, nao unachangia mtoto kuugua magonjwa ya zinaa, ukimwi na mimba za utotoni."

Simulizi nyingine inahusu mkasa wa mtoto mwenye ulemavu wa ngozi anayeishi mkoani Mara ni kutoka kwa mlemavu wa mguu mmoja, alioupata kutokana na unyanyasaji na ukatili uliofanywa na wasiojulikana, hata wakampatia ulemavu wa kudumu.

Kunatajwa kuwapo jitihada kubwa zinazochukuliwa na serikali nchini kutokomeza unyanyasaji, uonevu na ukatili kwa watoto, kwa kuanzishwa taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, kuwekwa sheria kali na kuchukuliwa hatua dhidi ya unyanyasaji au uonevu kwa watoto hao.

•



Shughuli za huduma ya kliniki zikiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

MAGONJWA YASIYOPEWA VIPAUMBELE...

# Trakoma: Maradhi yanayotisha hatima ya wengi kumudu kuona

- Serikali yajipanga 'stop' ifikapo 2030
- USAID yaahidi kuendelea 'kusapoti'

**Na Mwandishi Wetu**

KILA tarehe 30 ya Januari kila mwaka dunia inaadhimisha siku ya magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele. Nchini, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mwishoni mwa wiki iliyopita iliadhimisha siku hiyo mkoani Dodoma.

Magonjwa yanayotajwa hayakupewa kipaumbele nchini yanajumuisha usubi, kichocho, minyoo ya tumbo, trakoma au vikope, matende na mabusha. Lengo la maadhimisho ni kuangalia mafanikio yaliyopatikana na katika namna ya kutatua changamoto zilizopo.

Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kama Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) na Research Triangle Insitute International (RTI) wamechukua hatua kudhibiti magonjwa hayo, kukishuhudiwa mafanikio.

Hiyo ni hatua kwa kushirikiana na asasi ya USAID kuanzia mwaka 2010 hadi sasa, kuna ushuhuda wa mafanikio, asasi hiyo ikichangia Dola za Marekani bilioni moja (Sh. trilioni 2.3) kusaidia dawa za kupambana na magonjwa hayo na imeahidi kuendelea kusaidia.

Mratibu wa Kitengo Kinachopambana na Trakoma cha Mpango wa Taifa wa Kupambana na Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTDs), Ambakisye Mhiche, anaeleza undani wa ugonjwa huo, akianza na undani wa tafsiri yake.

Anafafanua trakoma au vikope, ni ugonjwa sugu unaoshambulia macho na kusababisha kope kupinda kugusa kioo cha jicho, haya husababisha makovu juu ya kioo cha jicho, chanzo kikuu ni bakteria anaowataja kwa jina 'Chlamydia Trachomatis.'

Mhiche anasema trakoma inapunguza uwezo wa kuona na hata kusababisha upofu usiotibika, pale isipochukuliwa hatua mapema na ndio unaoongoza duniani kusababisha upofu, ikikadiriwa zaidi ya watu milioni 154.5 duniani wameathirika na baadhi wako hatarini kuambukizwa.

**NAMNA UNAVYOSAMBAA**

Mhiche anaeleza ugonjwa huo unaenea kwa njia kuu mbili; kupitia inzi watokao kwenye mti wenye waadudu waambukizao, mambukizi kwenda kwa mwingine na njia ya pili, ni kwa kugusa au kutumia nguo, kitambaa, leso au taulo la mtu mwenye maambukizi, kisha kushika usoni

Anafafanua kwamba nchini taarifa za kuwapo trakoma zimekuwapo tangu mwanzoni mwa mwaka 1980 na inaelezwa kuwa miongoni mwa matatizo makubwa ya afya ya jamii katika sehemu kubwa nchini.

Pia, anasema mwanzoni mwa miaka ya 1990, trakoma ilikadiriwa kuchangia asilimia 26 au robo ya upofu nchini, katika mikoa iliyopo kanda ya kati ya nchi.

Tanzania kwa kushirikiana na wadau hasa Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la International Trakoma Innitiative (ITI) na USAID, ilichukua hatua kutathmini na kutambua ukubwa wa trakoma kitaifa, kati ya mwaka 2000 hadi 2012.

Anasema ilitambulika zaidi ya Watanzania milioni 12.5 kwenye halmashauri zaidi ya 71 wapo hatarini kupata maradhi ya vikope, wakati huohuo wapo zaidi ya watu milioni nne waliokwishaathirika, baadhi wako hatarini iwapo hakuna hatua stahiki za kuwasaidia kwa wakati sahihi.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Kunatajwa kuchukuliwa hatua kubwa kutokomeza trakoma, ambako katika jumla ya halmashauri 65 sawa na asilimia 91 ya malengo, ilifanyika hatua ya usawazishaji makope kutoka 167,000 hadi 27,000.

Ambakisye anasema, serikali inaendelea kushirikiana na wadau na sekta mbalimbali kuhakikisha huduma za maji usafi wa mazingia na vyoo inaimarishwa ili kuutokomeza ugonjwa huu katika hatua endelevu .



Msambazaji dawa kwenye jamii akiwa na kasha lake la dawa dhidi ya upofu, akiwa katika kazi ya kusambaza dawa vijijini. **PICHA: WHO.**



Daktari akiwa kazini kumhudumia mgonjwa wake. **PICHA: MTANDAO.**

Katika ngazi ya dunia, juhudi za kutokomeza ugonjwa wa vikope duniani zinaendelea, mwaka 1998 WHO ililipitisha Azimio la Kutokomeza Ugonjwa Trakoma Duniani ifikapo mwaka 2020.

Pia, kuna mkakati maalumu anaoutaja kwa jina SAFE (Surgery, Antibiotic, Face Washing and Environmental Improvement) yaani SAFI "Sawazisha Kope, Meza Dawa aina ya Antibaiotiki', Imarisha Usafi wa Uso na Mazingira, ili nchi wanachama walioathirika na vikope kuutokomeza.

Mhiche anaeleza malengo yalikuwa kufikia Desemba 2020, lakini takribani nchi 20 duniani ikiwamo Tanzania zilikuwa hazijafikia lengo la kutokomeza trakoma, kama walivyoelekezwa na WHO.

Mwaka huo shirika hilo la afya likaweka malengo mapya ya miaka 10 kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, ugonjwa wa trakoma na mengineyo yaliyokuwa hayapewi kipaumbele yanatokomezwa duniani.

**HISTORIA YA VIKOPE**

Mtaalamu huyo na Mratibu wa Magonjwa Yasiyopewa Vipaumbele anarejea historia inayoonyesha vikope vimekuwapo duniani kwa miaka mingi, ikitambulika rasmi tangu takribani miaka 10,000 Kabla ya Kristo, wakati binadamu walianza kuishi katika makundi kama jamii moja.

Anasema binadamu walianza kushambuliwa na vikope walipoanza shughuli za utafutaji mali kama vile kilimo, hali iliyowafanya kukusanyika sehemu moja kuunda jamii na kadri walivyoongezeka, hali ya afya na usafi ikazidi kudorórola, hivyo maambukizi yakasambaa kwa wengi zaidi.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, ugonjwa huo ulianza kujulikana zaidi katika jamii za mwanzo zilizoishi kuzunguka mito minne mikubwa kwenye mabonde ya Yangtze na Hwang nchini China, India Kusini mwa bara la Asia na Euphrates na Tigris maarufu kama Mesopotamia, kwenye mwambao wa Mto Nile, nchini Misri.

Aidha, Mhiche anasema kuna baadhi ya viashiria vinaonyesha uwapo wa vikope tangu miaka ya 2,700 Kabla ya Kristo ambako kunasemekana kufanyika upasuaji wa macho, kusawazisha kope zilizoathirika na ugonjwa wa trakoma.

Kwa kipindi chote hicho, anasema maradhi hayo hayakujulikana kama trakoma mpaka miaka ya 40 na 90 Baada ya Kristo, ndipo mwanasayansi wa Kigiriki ajulikanaye Dioscorides, alitumia kwa mara ya kwanza neno 'trachoma'.

Anasema baada ya hapo, kukawapo mijadala, uchambuzi na ugunduzi mwingi kuhusu vikope, hali iliyosababisha kutambulika zaidi miongoni mwa jamii za wataalamu wa afya duniani kote.

Anasema licha ya ugonjwa kujulikana tangu jamii za mwanzo kabisa za maisha ya binadamu, haukuweza kusambaa zaidi hadi karne ya 19, penye zama za mapunduzi ya viwanda, ambazo zina mwingiliano .

Miche anafafanua kuwa miaka 150 iliyopita, ugonjwa trakoma haukuwa tatizo kubwa barani Afrika, ikilinganishwa na Ulaya, pia Marekani.

AFYA

# Zahanati mpya kunusuru wajawazito Safari ya kilometa 30 ndani ya Ushetu

- Zawadi ya mnunuzi tumbaku kuirejesha faida
- Walitembea kwa hofu 'watoro' faini Sh. 50,000



.Mbunge wa jimbo la Ushetu mkoani Shinyanga Emmanuel Cherehani, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Misayu kata ya Ubagwe, kwenye uzinduzi wa zahanati yao npya **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

WANANCHI wanaoishi pembezoni mwa nchi, wamekuwa wakikutana na changamoto za ukosefu wa huduma za kiafya karibu na makazi yao, hali inayowafanya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za matibabu, hata wengine kukimbilia kwa waganga wa jadi kupata mbadala wa tiba.

Hatua hiyo imekuwa ikisababisha wajawazito kujifungua njiani ama majumbani na kuzalishwa na wananchi wasio na sifa za utabibu na imekuwa ikisababisha vifo vitokanavyo na uzazi usio salama kwa mjamzito kutokana na matumizi ya dawa nyingi wakati wa kujifungua.

Ndipo inapokuja simulizi ya kijiji cha Misayu, katika kata ya Ubagwe, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wananchi wanatembea umbali wa kilometa 30 kwenda na kurudi kutafuta huduma za matibabu katika zahanati ya Ubagwe, huku wajawazito wakishindwa kuhudhuria kiliniki, kama inavyotakiwa kiafya.

Pia wakati wa kipindi cha mvua za masika, barabara inayounganisha kijiji cha Misayo na zahanati ya Ubagwe, hujaa maji na kushindwa kupitika. Wengi wanashindwa kufika kituo cha afya ni lazima kujifungulia kwa wakunga wa jadi licha ya kutambua ni hatari sana kwao kiafya.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MAM), kila kijiji au kitongoji kinapaswa kuwa na Zahanati, hali kadhalika Kituo cha Afya kwa kila kata, wilaya inakuwa na Hospitali, mkoa Hospitali ya Rufani, hivyo hivyo hospitali za rufani za kanda na juu kuna Hospitali ya Taifa Muhimbili(MNH).

Ili kukabili shida iliyoko na umuhimu wa kujifungua katika zahanati na vituo vya afya, serikali za vijiji sita vinavyounda kata ya Ubagwe ziliweka tozo ya Sh.50,000 kwa mjamzito atakayebainika kujifungua nyumbani.

Kutokana na uhalisia wa faini hiyo na hali halisi kiuchumi, wajawazito wengi walalazimika kutembea umbali huo kufika Zahanati ya Ubagwe, ili kuepukana na faini hiyo.

**ZAHANATI MPYA RASMI**

Kwa wananchi wa kijiji cha Misayu kupata adha hiyo, kampuni ya ununuzi wa zao la Tumbaku ya JTI, imeamua kujenga zahanati mpya ya kisasa katika kijiji hicho, ili kutatua magumu ya wananchi hao kutembea umbali tajwa, fedha za ujenzi zikitokana na faida waliyoipata baada ya kununua na kuuza tumbaku.

Meneja wa JTI Kanda ya Ulyankulu na Ulowa, Joram Kissia, anasema walianza ujenzi wa zahanati hiyo Julai Mosi mwaka jana na ikakamilika mnamo Desemba 31 mwaka huo, kwa thamani ya Sh.milioni 289.135.

Hiyo ni baada ya kuona wananchi wanapata shida ya kutembea umbali mrefu kutafuta matibabu.

Kissia anasema, pia wametoa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.milioni 49.9 kwa zahanati hiyo mpya, ili ianze kutoa huduma kwa wananchi, huku serikali ikijiandaa kupeleka vifaa tiba, dawa na wakunga. Anaahidi wataendelea kutatua changamoto za kiafya, maji na elimu kwa wananchi hao.

Aidha, anasema zahanati hiyo ni ya kisasa zaidi na itakuwa inatoa huduma za mama na mtoto, wagonjwa wa nje, pia kuna nyumba ya Mganga Mfawidhi, ili awe karibu na kituo, hata inapotokea tatizo nyakati za usiku, iwe rahisi kufika katika zahanati na kutoa huduma kwa wananchi.



.Zahanati mpya iliyojengwa na kampuni ya ununuzi wa zao la Tumbaku - JTI kwa ajili ya kuwahudumia wakazi wa kijiji cha Misayu kata ya Ubagwe.

Meneja huyo anafafanua kwa kipindi cha mwaka jana zaidi ya Sh.milioni 527.94 zimetolewa katika miradi ya maendeleo ya afya, maji na elimu na bado mwaka huu kampuni hiyo inaendelea na kuchimba kisima kirefu cha maji safi na salama kijijini Nonwe na mradi uko katika hatua za mwisho na watakabidhi hivi karibuni.

**DMO USHETU AFAFANUA**

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu Nicodemus Senguo, anasema zahanati hiyo itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika zahanati ya Ubagwe, ambayo kwa siku inahudumia kati ya wagojwa 30 hadi 40 na kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu.

Anasema, zahanati ya Ubagwe kwa mwaka wanawake 22,000 hujifungua inayosababisha zahanati kuelemewa, hivyo hatua hiyo mpya inawasaidia na wengine kupata huduma ya karibu na makazi yao, wajawazito kudhuria kliniki kipindi chote cha ujauzito.

"Tumeshapokea vifaa vya kuanzia kutoa huduma kwa wananchi kutoka kampuni ya JTI na zahanati hii itaanza kutoa huduma hivi karibuni ili wananchi waache kutembea umbali wa kilometa 30 kwenda na kurudi kutafuta huduma za afya zahanati ya ubagwe" anasema Senguo.

**DED & MIPANGO YAKE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ushetu, Linno Mwageni, anasema wana jumla ya zahanati 23, vituo vya afya vitatu na hospitali moja ya wilaya na zote zinatoa huduma kwa wananchi, huku hali ya huduma kufikia umma ni asilimia 20 tu kwa sasa.

Anaendelea kusema, mwaka huu wameomba kusajili zahanati saba na zitaongeza huduma za matibabu kwa wananchi na kuongeza asilimia 29 za kiwango cha huduma, kila mwaka na watakuwa wanasajili zahanati sita lengo likiwa ni kusogeza huduma kwa wananchi na kuwaondolea changamoto zinazowakabili.

**MBUNGE USHETU/WEO**

Emmanuel Cherehani, anamtaka Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo Nicodemus Senguo, kutenga dirisha la wazee katika zahanati hiyo na kuwasimamia watoa huduma kuwa na lugha nzuri kwa wateja wao, kwani amekuwa akipokea malalamiko ya kauli zisizofaa za watoa huduma.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ubagwe, Andrew Mshobozi anasema, kuna jumla ya wakazi 20,870 na mwaka jana zaidi ya wajawazito 10 walilazimika kujifungulia njiani wakieleea zahanati, katika safari ya kuogopa kupigwa faini ya Sh.50,000.

Anasema, faini hiyo iliwekwa na viongozi wa serikali ya vijiji sita vinavyounda kata hiyo, kuhakikisha wajawazito wanahudhuria kliniki na kujifungua zahanati, lakini baadae ilifutwa na Diwani wa kata, baada ya kuona wananchi wake wanashindwa kumudu gharama hiyo.

**WAKAZI KICHEKO**

Mkazi wa Kijiji cha Ilamba Joyce Charles anasema,kabla ya kujengwa kwa zahanati hiyo walilazimika kutembea umbali wa kilometa 30 kwenda na kurudi kutafuta huduma za matibabu katika Zahanati ya Ubagwe hali ambayo wasiokuwa na uwezo walitumia miti shamba kujitibia.

Anasema,wajawazito walilazimika kutembea umbali huo kukwepa kutozwa faini ya Sh.50,000 iliyokuwa inatozwa kwa mjamzito atakayebainika kujifungulia nyumbani na kuzalishwa na mtu asiyekuwa na ujuzi na wengi wao walijifungulia njiani wakielekea zahanati hiyo.

"Ndugu yao alipata uchungu na kujifungulia njiani wakati tunamsindikiza kwenda kujifungua zahanati ya ubagwe,alijifungua salama lakini tulilazimika kupembea kondo la uzazi hadi kituoni ili tusipigwe faini ya Sh.50,000," anasema Charles.

Grace Mabula anasema, wengi walilazimika kukimbilia kwa waganga wa jadi kwa siri kupata matibabu, sasa kukamilika kwa zahanati imewasaidia kuondokana na changamoto hiyo na watahudhuria kiliniki vipindi vyao vyote nane vya ujauzito na kujifungulia kituoni.



# DC ataka waliofaulu kidato cha 1 kuripoti

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimwei, amewaagiza wazazi na walezi wenye watoto waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu kuhakikisha wanaripoti shule bila kisingizio cha kukosa sare na madaftari.

Onyo hiyo alilitoa juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Kikuyu Kusini jijini hapa.

Shekimweri alisema kuwa serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mikoa yote nchini na kwa wilaya hiyo madarasa 143 yameshajengwa na kukamilika na kuwekewa mahitaji yote yanayohitajika kwa wanafunzi na walimu.

"Hivyo hakuna kikwazo kwa wazazi na walezi wote wenye watoto ambao bado wamewaweka majumbani kwa kisingizio cha kushindwa kuwapeleka shule kutokana na kukosa sare kinachotakiwa wapelekwe kwanza na si vinginevyo," alisema.

Alisema suala la sare sio sababu ya kutokuwapeleka shule watoto waliochaguliwa kuanza elimu ya kidato cha kwanza wakati fedha nyingi zimetolewa ili wote wasome na kusiwapo hata mojawapo aliyefaulu akashindwa kupata elimu kwa kisingizio cha kukosa madarasa.

"Ninatoa agizo kwenu nyinyi wazazi na walezi wenye watoto mnaowaweka majumbani kwa kisingizio cha kukosa sare na mahitaji mengineyo, msiwakwamishe watoto wenu hao, badala yake wapelekeni shuleni masuala ya sare na madaftari hayo yatafuata baadaye," alisema.

Alisisitiza hataki kusikia au kuona mtoto yeyote ambaye amefaulu na kuchaguliwa kuanza kidato cha kwanza amekwamishwa na mzazi kwa kukalishwa nyumbani kwa madai kuwa hana sare za shule na madaftari.

"Tusipowapeleka shule watoto hao watakuwa wageni wa nani kwenye suala zima la uchumi, hata katika kupata kazi za ajira za kuajiriwa na kujiajiri maana zote hizo wanatakiwa vijana waliosoma kidato cha kwanza hadi vyuo vikuu na sivyo vinginevyo," alisema.

Pia aliwataka wananchi wa Dodoma kuwa na tabia ya kupanda miti na kuitunza kwenye maeneo yao wanayoishi ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani wakati wote.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, aliwaonya wananchi kuacha tabia ya ujenzi holela na uharibifu wa mazingira na kuwataka kufuata sheria zilizowekwa na Jiji hilo.

Mafuru alisema haitawafumbia macho na kuwaonea huruma kwa wale wanaojenga na kuharibu mazingira, hivyo wananchi wafuate taratibu na sheria zilizowekwa pindi wanapohitaji kujenga.

Aliwataka pia kutoa ushirikiano katika suala zima la ufanyaji wa usafi wa mazingira, badala ya kusubiri kushinikizwa.

# Gharama kipimo cha DNA yawekwa bayana

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amesema gharama za uchunguzi kwa kipimo cha vinasaba kwa mtu mmoja ni Sh.100,000.

Dk. Mafumiko alitoa ufafanuzi huo kwenye maonyesho ya Mahakama ya Tanzania yanayofanyika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyohitimishwa jana.

Alisema kumekuwapo na taarifa za upotoshaji kuhusu gharama hizo wakidai kuwa ni Sh. milioni mbili jambo ambalo si sahihi.

"Mara nyingi nimekuwa nikisikia gharama za Mkemia Mkuu wa Serikali za kuchukua hivi vipimo ni shilingi milioni mbili, shillingi 500,000, shilingi 700,000, hiyo ni taarifa ambayo siyo sahihi," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imebeba sehemu kubwa ya gharama za uchunguzi wa vinasaba, hivyo kuwezesha gharama ya uchunguzi kwa kipimo anachochukuliwa mtu mmoja kwa sasa kuwa Sh. 100,000.

"Kwa mfano, unataka kujua uhusiano wa baba, mama na mtoto. Pale tutachukua sampuli kutoka kwa watu watatu na gharama yake ni Sh. 300,000, lakini kukiwa kuna watoto wanne, watano, gharama yake itaongezeka hivyo hivyo, lakini, kwa kila tunayemchukua sampuli gharama yake ni Sh. 100,000," alifafanua Dk. Mafumiko.

Kwa mujibu wa mkemia huyo, kuna wakati fulani waliwahi kusema kuwa kwa kuangalia vitenganishi vyake, gharama ya kipimo ingekuwa kati ya Sh.700,000 hadi 800,000 kama serikali isingebeba sehemu ya gharama hizo, lakini hadi sasa bado ofisi yake inatoza gharama ile ile ya Sh. 100,000 kwa kila wanayemchukua sampuli.

Alitoa wito kwa wananchi wanapotaka kufanya kipimo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kinachohusiana na masuala ya kijinai kutumia mamlaka zilizoko badala ya wao wenyewe kama wateja kwenda moja kwa moja katika ofisi hiyo.

"Kuna mamlaka zilizowekwa kwa ajili ya kumwomba Mkemia Mkuu wa Serikali vipimo. Kama ni suala la kijamii kuna maofisa ustawi wa jamii, kuna mawakili walioandikishwa, kama ni suala lipo mahakamani kuna mahakama na wenzetu wa Jeshi la Polisi, kama ni suala la kimatibabu kuna madaktari, kama suala la majanga, kuna wa wilaya," alisema.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Wizara ya Mambo ya Ndani, Marlin Komba (kushoto), akijadiliana jambo na Kamishna wa Polisi Utawala na Rasilimali Watu, CP Benedict Wakulyamba, kabla ya kuanza kwa kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: WMNN**

# Uingereza, Tanzania zajadili uwekezaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amefanya mazungumzo na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, kwa lengo la kuendeleza ushirikiano na kukuza uwekezaji na biashara kati ya nchi hizo.

Akizungumza jana na Balozi wa Uingereza katika ofisi za wizara hiyo jijini hapa, Dk. Kijaji alisema Tanzania itaendelea kushirikiana na Uingereza kutekeleza maazimio ya Mkutano wa Serikali kwa Serikali (G2G) yaliolenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Uingereza.

Kwa upande wake, Balozi Concar alisema kuwa Serikali ya Uingereza itaendelea kutekeleza maazimio hayo kwa kushirikiana na Tanzania katika kutekeleza mpango kazi jumuishi.

Alibainisha kuwa mpango huo unalenga kuziwezesha taasisi za umma na binafsi zinazohusika na uwekezaji na biashara kupanga vipaumbele vya kibiashara vinavyotekelezeka kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali yanayoweza kujitokeza.

Kongamano la Biashara na Uwekezaji kati ya Tanzania na Uingereza lilifanyika Novemba 16, 2021, Dar es Salaam na lililenga kupanua zaidi wigo wa ushirikiano katika maeneo ya biashara na uwekezaji hususan sekta za nishati, madini, miundombinu, kilimo, uchumi wa bluu na utalii, kuhamasisha wafanyabiashara wa Uingereza kuja kuwekeza nchini na wafanyabiashara wa Tanzania kuuza bidhaa zao Uingereza.



# Tanzania, Malawi zajadili matumizi ya meli

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI za Tanzania na Malawi, zimeanza mazungumzo yanayolenga kuruhusu meli za abiria na mizigo zilizoko katika Ziwa Nyasa kutia nanga kwenye bandari za pande zote mbili ili kuchochea uchumi wa nchi hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo alipokuwa anazindua tena safari za meli ya MV- Mbeya II ambayo ilisitisha safari zake ili kupisha matengenezo baada ya kupigwa na dhoruba miezi tisa iliyopita.

Meli hiyo ilipigwa na dhoruba katika eneo la ufukwe wa Matema ikiwa na abiria zaidi ya 80 na kuharibika baadhi ya mifumo ikiwemo injini ya kulia hali ambayo ililazimu Serikali kumuagiza mkandarasi wa Kampuni ya Songoro Marine kuifanyia matengenezo.

Alisema zipo bidhaa za Tanzania ambazo zinahitajika Malawi, lakini hulazimika kusafirishwa kwa njia ya barabara kwa sababu ya kutokuwepo kwa ushirikiano wa usafiri wa majini.

Alisema zipo Meli za Tanzania ambazo zimejengwa na Serikali kwa gharama kubwa lakini hazifanyi kazi ipasavyo lakini mazungumzo hayo yakikamilika zitafanya kazi vizuri.

"Ninachoomba ni uadilifu kwa manahodha wetu na wafanyakazi wote wa meli, mfanye kazi kwa weledi ili kwa pamoja tufanikishe azma ya serikali ya kuzijenga meli hizi, tukisafirisha mizigo kwa njia ya maji tutanusuru hata barabara zetu" alisema Homera.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, alisema tangu meli ya MV-Mbeya II ilipositisha safari zake, wananchi wa wilaya hiyo wamepata shida na hata baadhi ya shughuli za kiuchumi zilikuwa hazifanyiki vizuri.

Alisema wananchi walikuwa wanalazimika kusafiri kwa kutumia vyombo ambavyo usalama wake sio wa uhakika kama ilivyo meli na hivyo akaishukuru Serikali kwa kufufua meli hiyo.

"Kuna baadhi walikuwa wanasafiri kwa kutumia mitumbwi na majahazi, vyombo ambavyo uhakika wa usalama wake sio wa uhakika, sasa naamini kwa kuzinduliwa tena safari za meli yetu hii wananchi wanafungua ukurasa mpya wa maisha," alisema Mlawa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema usafiri wa meli ni wa haraka zaidi kuliko majahazi na mitumbwi na kwamba hata gharama yake ni nafuu kwa wananchi.

Alisema usafiri huo utasaidia kuongeza kasi ya maendeleo kwa wananchi wa maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Nyasa huku akisisitiza kuwa Serikali ina mipango ya kuboresha miundombinu ya barabara.

Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Nyasa, Abdallah Mohamed, alisema Meli hiyo ilipigwa na dhoruba Mei 3 mwaka jana na ikaharibika baadhi ya mifumo.

Alisema kwa sasa meli hiyo imefanyiwa matengenezo na kufanyiwa majaribio baada ya kukaguliwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) ambalo wataalamu wake walisema iko sawa.

Alisema meli hiyo ni kiunganishi muhimu kati ya wananchi wa maeneo yote ya mwambao mwa Ziwa Nyasa, hivyo akawataka wananchi waliokuwa wanahangaika usafiri kuanza tena kuitumia meli hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), akishirikiana na viongozi mbalimbali kukata utepe kuzindua safari za meli ya MV-Mbeya II, kwenye Bandari ya Kiwira, wilayani Kyera, mkoani humo juzi. Meli hiyo, ilisitisha huduma kwa takribani miezi tisa kwa ajili ya ukarabati, baada ya kupigwa na dhoruba na kuharibika baadhi ya mifumo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TARI yaja na mbegu mpya za maharage kukabili tabianchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo, wamezalisha mbegu mpya za maharage ambazo zina uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha mbegu hizo zinadaiwa kuwa na uwezo wa kuzaa sana tofauti na zile za asili na hivyo kuwa na uwezo wa kuwainua wakulima kiuchumi na kuwahakikishia usalama wa chakula.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha wadau wa kilimo cha maharage kutoka katika mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini cha kutathimni mbegu mpya za maharage.

Dk. Bucheyeki alisema mbegu hizo zina uwezo wa kuhimili magonjwa na hali mbaya ya hewa ikiwemo mvua nyingi na hata ukame hivyo akasisitiza kuwa uzalishaji wake hauna gharama kubwa ikilinganishwa na aina zingine.

Alisema mbegu hizo zinaanza kufanyiwa majaribio katika wilaya 10 za mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kabla ya kuanza kusambazwa kwa wakulima wa mikoa mingine.

"Sasa hivi tunaenda kidigitali zaidi, hizi mbegu tunazifanyia tathimini kila mdau kwa njia anazojua yeye, lakini leo tunafanya tathimini ya pamoja ili tuwe na uhakika wa kile tunachowapelekea wakulima," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kwa sasa kilimo kinahitaji kuwa na teknolojia ya kisasa ili kiwe na tija kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa sasa yanaitesa dunia .

# Wataka maboresho ya barabara Shizuvi-Ilembo Chunya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Shizuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba Serikali kuwaboreshea barabara inayoounganisha Kata hiyo na Kata ya Ilembo ili kuwarahishia mawasiliano hasa kipindi hiki cha mvua ambacho walisema haipitiki kabisa.

Walitoa kilio hicho wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachu, na kufanyika katika kijiji cha Inyala-Ilembo ambapo walisema barabara hiyo ni kero yao ya muda mrefu na inakwamisha maendeleo.

Mmoja wa wananchi hao, Mariam Mwamahonje, alisema wanawake ndio wanaopata shida zaidi ya barabara hiyo hasa wanapotakiwa kwenda kujifungulia kwenye Kituo cha Afya cha Ilembo.

Alisema katika Kijiji chao ipo Zahanati lakini wakati mwingine huwa inashindikana kujifungulia hapo na wanapewa rufani ya kwenda kujifungulia Ilembo ambako alisema ni mbali na barabara yao imekuwa ikiwaongezea matatizo.

Alisema wanapopewa rufani ya kwenda kujifungulia Ilembo huwa wanasafirishwa kwa pikipiki jambo ambalo alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo matatizo huwa yanaongezeka zaidi na wakati mwingine huwa wanaumia.

Alisema huwa wanaanguka na pikipiki, hivyo kufika kituo cha afya wakiwa wamechoka na hivyo kujifungua kwa shida kutokana na uchovu unaosababishwa na ubovu wa barabara.

"Wakati mwingine mwanamke anajifungua kabla ya wakati kutokana na kurushwarushwa na pikipiki, wengine wanapata shida kujifungua kwa sababu wanakuwa wamechoka, sasa tunaomba utufikishie salamu kwa rais wetu Samia atuonee huruma wanawake wenzake," alisema Mariam.

Naye Sophia Shila alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo wanatumia gharama kubwa kusafirisha bidhaa hali ambayo inasababisha hata bei kuongezeka.

Alisema wajasiriamali wa eneo hilo wananunua bidhaa kama nyanya katika soko la Ilembo lakini usafirishaji wake ni mgumu kutokana na ubovu huo wa barabara ambapo alisema nyanya za Sh. 10,000 zinasafirishwa kwa Sh. 8,000.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, aliiomba Serikali kuipandisha hadhi barabara hiyo ili badala ya kusimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) isimamiwe na Wakala wa Bararara Taanzania (TANROADS).

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa sababu inaunganisha Kata mbili za Wilaya ya Ileje na tatu za Wilaya ya Mbeya na hivyo ni muhimu kwa maendeleo ya pande hizo mbili.

"Hili eneo ni miongoni mwa maeneo muhimu sana kiuchumi, wananchi wa huku ni wakulima wazuri sana, lakini tatizo hili la barabara linawaathiri sana hivyo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya tunaomba ipandishwe hadhi," alisema Njeza.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Chuachua, aliahidi kushughulikia tatizo hilo kwa kuwaagiza TARURA kuikarabati ili iwe inapitika mwaka mzima badala ya kupitika kipindi cha kiangazi pekee.

Alisema mbali na barabara hiyo pia zipo barabara zingine za wilaya hiyo ambazo miundombinu yake sio mizuri hasa kipindi hiki cha mvua na hivyo akasisitiza kuwa atawaagiza TARURA kuziweka kwenye vipaumbele vya ujenzi.



## Norway kusaidia utafiti tiba asilia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Norway imesema ipo tayari kusaidia kazi za utafiti wa miti shamba kutibu tiba asilia za maradhi mbalimbali hatari ambayo yamekuwa yakisababisha vifo vingi.

Balozi wa Norway nchini, Elizabeth Jacobsen, aliyasema hayo jana alipozungumza na uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, ukiongozwa na Waziri Nassor Ahmed Mazrui ofisini kwake Mnazi Mmoja, Unguja.

Alisema miti shamba imekuwa ikitumika katika kutoa tiba na utafiti wa maradhi katika nchi nyingi na hivyo kutoa ahueni kubwa.

Alisema Norway ipo tayari kuleta wataalamu watakaosaidia kufanya kazi za utaalamu katika miti shamba kutoa tiba ya maradhi mbalimbali.

"Serikali ya Norway ipo tayari kusaidia kazi za utafiti wa miti shamba kwa ajili ya kutoa tiba asilia kupambana na maradhi mbalimbali hatari yanayotishia afya za wananchi," aliahidi.

Alibainisha kufurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuwapatia makazi bora na huduma zote wazee ambao mchango wao kwa taifa na familia ni mkubwa.

Waziri Mazrui aliipongeza Serikali ya Norway kwa juhudi zake kubwa za kusaidia maendeleo ya Zanzibar na kujikita katika sekta ya afya na wazee.

Alisema Norway inaingiza fedha nyingi katika miradi ya kimataifa ambayo husaidia katika sekta ya wazee, watoto pamoja na wanawake.

Mazrui alimwomba Balozi wa Norway kuipatia Zanzibar mashine ya kuangalia saratani ya matiti kwa wanawake, akisisitiza kuwa maradhi hayo ni tishio kwa kundi la wanawake wakiwamo wanafunzi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaridhishwa na misaada inayotolewa na Norway ambayo imejikita katika sekta ya afya kwa watoto, wanawake na wazee pamoja na upatikanaji wa dawa muhimu," alisifu.

Taasisi ya utafiti wa maradhi iliyoko Binguni Wilaya ya Kati Unguja, imeanza kufanya utafiti wa miti shamba kwa ajili ya kutibu maradhi mbalimbali ikiwamo matumizi ya kujifukiza, maarufu kupiga nyungu katika kupambana na ugonjwa wa UVIKO-19.

# Makosa 1,100 yatua polisi mwaka mmoja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKOSA 1,161 dhidi ya binadamu yameripotiwa polisi Zanzibar kwa mwaka 2021 yakiwamo ya udhalilishaji na mauaji, sawa na ongezeko la makosa 204 kulinganishwa na makosa 957 ya mwaka 2020.

Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai Zanzibar, Zuberi Chembela, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kilimani, Zanzibar kuhusu hali ya usalama na matukio yaliyoripotiwa.

Alisema kuongezeka kwa makosa hayo kunatokana na wananchi kupata uelewa na mwamko wa kuyaripoti matukio hayo tofauti na ilivyokuwa awali.

Kuhusu mauaji, alisema jumla ya matukio 41 yaliripotiwa mwaka 2021 kulinganishwa na matukio 33 yaliyoripotiwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la matukio manane.

Alisema kuwa matukio ya makosa ya kuwania mali ambayo yanajumuisha makosa ya unyang'anyi wa kutumia nguvu, uvunjaji, wizi wa pikipiki, wizi wa mazao, mifugo, fedha bandia na mengineyo ni 1,666 kwa mwaka 2021.

"Makosa hayo 1,666 ni upungufu wa makosa 410 yaliyoripotiwa mwaka 2020 ambayo makosa yote yalikuwa 2,076," alisema Chembela.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kuwaripoti wahalifu wa matukio mbalimbali na kutosita kutoa ushahidi jeshi hilo linapofanya uchunguzi wa matukio hayo.

Alibainisha vikwazo vikubwa vinavyolikabili jeshi hilo ni pamoja na muhali kwa kuwa wahalifu wa matukio hayo hasa ya udhalilishaji ni watu wanaofahamika katika jamii na watu wa karibu katika familia za waliodhalilishwa.

"Bado muhali umetawala katika jamii hasa kwa matukio haya ya udhalilishaji, tunapofanya upelelezi wa kesi hizi tunakosa ushirikiano wa jamii kutokana na kuwaonea aibu wahalifu hao kwa kuwa ni watu wa karibu katika familia," alisema.

Alibainisha kuwa hali ya usalama kwa sasa ni nzuri na wananchi wanaendelea na shughuli zao za kujitafutia maendeleo na hakuna tukio lolote lililojitokeza ambalo limeleta fadhaiko kwa wananchi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga (kulia), akikabidhi cheti kwa mhitimu Asma Makame Haji, wakati wa mahafali ya chuo cha Microtech Institute of Business Technology, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Gharama ya ukodishaji visiwa yatangazwa 19

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Soraga, amesema gharama za ukodishwaji wa visiwa 10 vilivyokodishwa kwa wawekezaji ni zaidi ya dola milioni 260.

Aliyasema hayo jana alipotoa ufafanuzi kuhusu ukodishwaji wa visiwa hivyo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mwanakwerekwe, Zanzibar.

Waziri huyo alisema Serikali ya Zanzibar imekodisha visiwa hivyo kwa ajili ya kukuza sekta ya utalii na kupata mapato yatokanayo na visiwa hivyo kwa kuwa ilikuwa hainufaiki na uwapo wa visiwa hivyo.

Alibainisha kuwa hadi sasa fedha zilizolipwa kwa ajili ya ukodishwaji wa visiwa hivyo 10 vilivyotangazwa na serikali ni zaidi ya dola milioni 14.

Alisema kuwa fedha hizo zilizolipwa na nyingine ambazo zitalipwa zitatumika kwa shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo uboreshaji wa huduma za kijamii.

Waziri huyo alisema katika ukodishaji wa visiwa hivyo suala la utunzaji wa mazingira limezingatiwa na ni marufuku kwa wawekezaji kutumia saruji au matofali na badala yake watumie mbao katika ujenzi wa hoteli katika visiwa hivyo.

Alibainisha kuwa katika visiwa hivyo vilivyokodishwa bado umeme wa gridi ya taifa haujafika, hivyo wawekezaji hao watatumia nishati ya umeme mbadala ambao ni umeme wa jua ulio rafiki mzuri kwa utunzaji wa mazingira.

Alisema serikali inafahamu kwamba baadhi ya visiwa vilivyokodishwa kuna harakati za kijamii zinazofanywa na wananchi ikiwamo uvuvi hivyo hakuna atakayezuiwa au kufukuzwa kuendelea na shughuli hizo.

Alisema wanatarajia kupita katika vijiji vilivyokaribu na visiwa hivyo 10 vilivyokodishwa kwa awamu ya kwanza kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhamira ya serikali kukodisha visiwa hivyo ili kuondosha kasumba zilizoenea mitaani kuhusu uamuzi huo wa serikali.

Hivi karibu akizungumza na waandishi wa habari, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema visiwa vinne vilivyokodishwa awali serikali haikufaidika kwa sababu ilikuwa ikitoza kodi ya ardhi pekee ambayo ni fedha ndogo na kuvitaja visiwa hivyo ni Bawe, Mnemba, Chumbe na Vision Island ambavyo sasa vimeingia katika visiwa 10 vilivyokodishwa kwa wawekezaji.

Alibainisha kwamba serikali tayari imeshatangaza visiwa vingine 10, hivyo ni matarajio kwamba wawekezaji wengine watajitokeza kuwekeza katika visiwa hivyo kama zilivyo nchi zingine duniani.

Visiwa 10 vilivyokodishwa kwa wawekezaji ni Njao, Matumbini, Misali, Bawe, Changuu, Kwale, Pamunda A na B, Chwapwani na Chumbe.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya NZEGA**
**Kituo cha IGUSULE mkoa wa TABORA**
**Usimamizi wa miorathi na 1/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHABANI MZEE MAGANGA WA BOMBANI IGUSULE NZEGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA SOPHIA SHABANI MZEE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni ya usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18/2/2022 kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia:endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 26/1/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
IGUSULE – NZEGA
67

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**HAPPYNESS JOSEPH MAMAIDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 520 DMK aina ya TOYOTA VANGUARD ,chasis namba aca335132326,engine namba 2az2827794,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha poliosi Polisi taarifa**ARU/ARU/ RB/38211/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MALEMBO D. SILAS** Anatangaza kupotelewa na cheti chakuhitimu kidato cha nne index **No S1877-0057** kilichotolewa na **DR. NCHIMBI SECONDRY SCHOOL** Mwaka 2014. cheti cha chuo **NTA Level 6 No. 0089479** kilichotoleawa na **SHIRATI COLLEGE OF HEALTH SCIENCES** mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa polisi: **MAR/BUN/RB/562736/2021.**

## KUPOTEA KWA PASPORT



**FILBERT FRANCIS TEMBA**
Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye no, TAE 154092 iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji Mwaka 2019 Dar Es Salaam.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**KL/MOS/RB/45517/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GLORY SIMON MOSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba S.3068/0034 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia RASESA SEKONDARI mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/MAG/RB/279660/2021.

## JKUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SUNDAY LESTON MWASENGA**
Anatangaza kupotea kwa kadi yake ya Pikipiki yenye jina la **NETA LESTON MWASENGA** no za usajili **MC 471CRS CHASES NO. md2b15bx71we90495, ENGINE NO. jvxwle02486** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi.
**DOD/DOD/RB/49152/2022**

## TANGAZO KUPOTEA HATI YA KIWANJA

John Edward Mwangosi mkazi wa Salasala, Kinondoni, mkoa wa Daressalaam. Anatangaza kupotelewa na Hati ya Kiwanja chenye namba 10755. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo Karibu au awasiliane na John Mwangosi kwa simu namba 0784540998. RB namba KW/RB/5993/2021 control namba 9910831096317.

## TANGAZO!!
## AFRIWELD INDUSTRIES LTD
## Nafasi ya kazi

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35
**Nafasi:** Mauzo
MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!!
wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!
Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**
Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni
**01/01/2022 MPAKA 15/02/2022**
**Asante**
116653602

## KUPOTEA KWA CHETI



**LIGHTNESS J. NGULO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne. Chenye namba S.1062.0053 kilichotolewa na Baraza la Mtihani wa Taifa kwa mtihani wa mwaka 2018 katika shule ya sekondari MALENGA. Ka yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi namba **MBE/MBE/RB/355281/2021**

*Uza,*
*Chenye Thamani*
*Kubwa Kwa*
*Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*
*Tupigie*
*0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

# Mwanajeshi apata cheo baada ya kumsaidia mama kujifungua

**Lusaka,** ZAMBIA

MWANAJESHI amepandishwa cheo cha kijeshi kwa kumsaidia mwanamke kujifungua mtoto katika shamba la mahindi.

Humphrey Mangisani, amepadishwa cheo kutoka askari asiye na cheo hadi koplo kamili kwa ujasiri wake.

Tukio la kuzaliwa kwa mtoto huyo, kwa mujibu wa taarifa kutoka Zambia, lilitokea wiki iliyopita katika Wilaya ya Mashariki mwa nchi, Petauke.

Koplo Mangisani, alisema aliitwa kumsaidia mwanamke huyo ambaye alikuwa amepata uchungu wa uzazi.

Alimtafutia pikipiki ya bodaboda ambayo ilimpeleka hospitali na kumfuata nyuma na bodaboda nyingine, ili kufuatilia hali yake.

Alisema ingawa uchungu wake ulikuwa wa haraka, kiasi alilazimika kuweka kando pikipiki na kumsaidia kujifungua mtoto katika shamba moja la mahindi, lililoko kando ya barabara.

"Nilitafuta na kupata wembe haraka na kumsaidia kukata kitovu. Mvua ilikuwa inanyesha alipojifungua. Nikamchukua mtoto haraka nikampeleka hospitalini na mama yake akafuata nyuma," alisema.

**BBC**

# 25 wafariki kwa umeme, shambulio DRC

**Kinshasa,** DRC

POLISI Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imesema watu 25 wamefariki dunia, baada ya waya unaopeleka umeme wenye nguvu kukatika na kuanguka kwenye nyumba na soko katika kitongoji cha mji mkuu Kinshasa.

"Waya wa umeme wenye nguvu ulianguka kwenye nyumba kadhaa katika Wilaya ya Matadi-Kibala na kwenye soko, watu kadhaa walifariki papo hapo," Mkuu wa Polisi Kinshasa, Sylvano Kasongo, alisema.

Video kutoka sokoni ambazo zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha watu wakiomboleza kando ya miili kadhaa, ikiwa imelala kwenye madimbwi ya maji ambapo watu hao walifia.

Shirika la habari la Reuters halikuweza kuthibitisha video hizo.

Wakati huohuo mjini Beni, watu wameripotiwa kuuawa kwenye shambulia Mashariki mwa DRC, jana, kwa mujibu wa kambi ya makazi na kundi la msaada wa kiutu.

Vyanzo vya taarifa viliiarifu Reuters kwamba kikosi cha CODECO kinadaiwa kuhusika na tukio hilo lililotokea kambi ya Savo, Jimbo la Ituri.

Msemaji wa Jeshi Ituri, Jules Ngongo alithibitisha tukio hilo akidai CODECO kuhusika na kwamba 20 waliuawa.

**VOA**

# Kimbunga chaathiri shule 800 nchini Msumbiji

**Maputo,** MSUMBIJI

TAKRIBANI shule 800 zimeharibiwa na kimbunga Ana wiki iliyopita, Wizara ya Elimu, imesema.

Mahema yamewekwa kutumika kama madarasa ya muda kwa wanafunzi wapatao 300,000 na walimu 4,700 walioathiriwa.

Kimbunga Ana, kiligonga Kusini mwa Afrika wiki iliyopita na kuua zaidi ya watu 80 na kuwaacha maelfu ya watu bila makazi.

Kanda hiyo sasa inajiandaa kwa kimbunga cha pili kinachotarajiwa kutua baadaye wiki hii.

Wataalamu wa utabiri wa hali ya hewa, walisema kimbunga cha tropiki kiitwacho Batsirai, kiliongeza kasi yake Jumanne wiki hii, huku Mauritius ikitoa onyo la kiwango cha tatu, kiwango cha pili cha juu cha tahadhari ya hali ya hewa.

Familia nyingi katika kisiwa cha Bahari ya Hindi, zimekuwa zikikimbilia madukani ili kuhifadhi chakula na zimeambiwa zisiende baharini.

Usafishaji wa maeneo unaendelea katika majimbo ya Manica, Nampula Sofala, Tete na Zambézia, ambako shule 778 ziliharibiwa na kimbunga Ana.

Gina Guibunda, Msemaji wa Wizara ya Elimu, alitoa tangazo hilo mwanzoni mwa mwaka wa masomo wa Msumbiji.

**BBC**



Karen Maite (16), akisaidiwa na watoa huduma za msaada eneo ambalo kulitokea maporomoko ya udongo, mjini Quito, nchini Ecuador, juzi. Takribani watu 24 walipoteza maisha kwenye tukio hilo, na wengine 12 hawajulikani waliko. **PICHA: REUTERS**

# Jaribio mapinduzi limedhibitiwa: Rais Embalo

**Bissau,** GUINEA BISSAU

RAIS wa Guinea-Bissau, Umaro Sissoco Embalo, amewaambia waandishi wa habari Jumanne kwamba, baada ya sintofahamu kuripotiwa kuhusu nchi kupinduliwa, akidai limeshindwa.

Milio ya risasi ilisikika katikati mwa mji huo karibu na taasisi za nchi. Milipuko iliyosababisha wakazi kupatwa na hofu.

Rais Embalo alionekana mbele ya waandishi wa habari Jumanne jioni, baada ya saa kadhaa ya sintofahamu katika mji mkuu wa Guinea-Bissau.

Akiwa amezungukwa na Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Sheria, Rais Embalo, alivishukuru vikosi vya ulinzi na usalama vya nchi hiyo, kwa kuzuia mapinduzi hayo ambayo lengo ilikuwa ni kuhatarisha demokrasia.

"Kilikuwa ni kitendo kilichoandaliwa na kupangwa," alisema Rais wa Guinea-Bissau, ambaye alihusisha jaribio hili la mapinduzi na maamuzi aliyoyachukua hususan mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya na ufisadi, bila kutaja wazi wahusika wa mapinduzi hayo.

"Washambuliaji waliweza kuzungumza nami kabla ya matukio haya ya umwagaji damu, ambayo yamesababisha vifo vya watu kadhaa na wengine kujeruhiwa vibaya," alisisitiza Rais Embalo, bila hata hivyo kutaja idadi ya watu waliouawa.

Kiongozi huyo, alidai kulikuwa na mpango wa kumuua yeye na Baraza lake la Mawaziri na watu waliojihami kwa kile anachosema ni kutokana na juhudi zake za kupambana na ufisadi na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guteress, alilaani kilichotokea nchini Guinea Bissau na kutaka taasisi ya kidemokrasia kuheshimiwa.

Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), imeshtumu pia jaribio hilo la mapinduzi. Kwa sasa hali inaelezwa kuwa tulivu.

**RFI**

# SERIKALI KAMILI KUSAKA VIPAJI MTAA KWA MTAA

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

SERIKALI imesema itasaka vipaji vya vijana mtaa kwa mtaa, kata kwa kata, wilaya kwa wilaya na mkoa kwa mkoa ili kuwaibua kwa lengo la kuonyesha uwezo wao pamoja na kujiajiri.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Sylivia Sigula, mpango wa serikali kwenye kuibua na kutumia vipaji vya vijana nchini.

Alisema ni jukumu la serikali kukuza na kuendeleza sanaa na kwamba kuna vijana wenye vipaji, ila wanashindwa kuvitumia kwa sababu ya mazingira magumu, pamoja na kushirikiana na sekta binafsi kuwa na matamasha.

Akijibu swali hilo, Mchengerwa alisema:

"Tumejipanga vizuri na kuna mfumo maalumu kwenye mitaa, wilaya na mkoa kusaka vijana wenye vipaji, na kila jambo litakuwa na uzito wake na kila kinachohusu sekta hiyo kitapewa uzito.Tuna shule 56 za kuendeleza vipaji nchini."

Awali, akijibu swali la msingi la Mbunge huyo aliyetaka kujua mpango wa serikali wa kutoa ajira rasmi na zisizo rasmi kupitia tasnia ya sanaa, waziri huyo alisema ili kukamilisha hilo serikali itafanya mambo matano.

Mchengerwa aliyataja kuwa ni kuhakikisha vifaa na vitendea kazi vya sanaa vinapatikana kwa bei nafuu kwa kufanya mapitio kwenye kodi za vifaa hivyo.

Jingine kupitia upya tozo kwenye Kanuni za BASATA, COSOTA na Bodi ya Filamu Tanzania ili ziwe Rafiki kwa walipaji.

Pia, kuanzisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya usajili, maombi ya vibali na leseni pamoja na mfumo rasmi wa ukusanyaji mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za Sanaa.

Jingine ni kujenga miundombinu ya sanaa kama vile Arts Arena, National Art Gallery na One Stop Center.

Pia, kuanzisha mfuko utakaokuwa suluhisho la kimitaji na mafunzo kwa wadau wa sekta ya sanaa.




Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, akionyesha jezi feki za Yanga zilizokamatwa katika maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi yakamata jezi feki 1,700

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, linawashikilia watu 17 baada ya kukutwa na jezi feki 1,708 za Yanga inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao wamekamatwa kwa nyakati tofauti katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mwanza na Zanzibar.

Muliro aliwataja watuhumiwa hao ni Zahiri Hassan (17) anayedaiwa kukutwa katika eneo la Uwanja wa Benjamin Mkapa akiwa na jezi 52.

"Katika mtaa wa Agrey, Kariakoo alikamatwa, Majibu Ndahya akiwa na jezi 124, Mohamed Ramadhani (jezi 86), John Stanslaus (jezi 39) na Emanuel Kinasa aliyekutwa na jezi 60.

Aliongeza watuhumiwa hao waliwataja wenzao kutoka Zanzibar ambao walikamatwa katika Uwanja wa Amani wakiwa na jezi 36 huku akisema jezi nyingine 134 zilipatikana kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Mkoa wa Tanga huku nyingine 811 zilikamatwa Mwanza na jumla ya watuhumiwa tisa wanashikiliwa kwa kosa hilo.

"Jeshi la Polisi linawakumbusha wale wote wanaojihusisha na vitendo hivi vya kutengeneza, kusambaza na kuuza bidhaa hizi kwa kuiga au kufananisha nembo ya bidhaa ya mtu mwingine iliyosajiliwa kisheria kuwa ni kinyume cha sheria," Murilo alisema.

Aliongeza kwa sasa wanaendelea kuwasiliana na mamlaka nyingine za kisheria ili watuhumiwa hao wachukuliwe hatua zinazostahili.

## Nyoso, Lyanga kuikabili Polisi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikijiandaa kucheza dhidi ya Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Jumapili, nyota watatu wa Geita Gold FC, Danny Lyanga, Jeremiah Rubanguka na Juma Nyoso ambao walikuwa wajeruhi, wameanza mazoezi na wako tayari kwa mchezo huo.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana inasema Nyoso na Lyanga afya zao zimeimarika na watakuwa sehemu ya kikosi kitakachoivaa Polisi Tanzania.

Taarifa hiyo ilimtaja Rubanguka pekee ndiyo hatacheza mechi hiyo kwa sababu ya kuchelewa kuanza mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake, hivyo mwalimu amempa muda zaidi wa kujiimarisha.

Lyanga alipata maumivu ya nyama za paja katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Dodoma Jiji iliyochezwa Januari 15, mwaka huu ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1.

"Juma Nyoso alipasuka paji la uso katika mechi hiyo hiyo dhidi ya Dodoma Jiji, sasa ameshapona na ameanza mazoezi tayari. Jeremiah Rubanduka alipata maumivu ya nyonga kwenye mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Tunduru Korosho, amepata matibabu, anaendelea vizuri," iliongeza sehemu ya taarifa hiyo.

## Kisiwani, Kipanga, JKU, Sailor vitani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI KUU Zanzibar inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa JKU kuwavaa Black Sailor kwenye Uwanja wa Amaani wakati Kisiwani watawakaribisha 'Maafande' wa Kipanga kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

Ligi hiyo inarejea tena baada ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum, alisema tayari bodi hiyo imeshatoa ratiba na klabu zote 16 zinatakiwa kuendelea na maandalizi kwa ajili ya kushuka dimbani kuwania pointi tatu muhimu.

"Bodi ya ligi imeshatoa ratiba yake ya kuendelea na Ligi Kuu, huku ligi daraja la kwanza Kanda pia inaendelea, kama tunavyojua ratiba imetolewa kwa kuangalia mwezi wa ramadhani, kwa kawaida Zanzibar ligi zote husimama ili kupisha mwezi huo mtukufu," alisema Salum.

Aliongeza katika kuhakikisha wanakabiliana na changamoto ya ratiba hiyo iliyotolewa, bodi hiyo imepanga kukutana na viongozi wa timu zote ili kuangalia namna watakavyotangua changamoto zilizojitokeza hususani za usafiri.

"Kuna malalamiko kuhusiana na timu moja kukaa muda mrefu katika kituo hali ya kuwa hawana uwezo wa kujikimu," alisema kiongozi huyo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY KUMSHAWISHI HAALAND

MANCHESTER City "itafanya kila iwezalo" kumshawishi mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland (21), ili kujiunga na klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu, licha ya nyota huyo wa Norway kuonekana anataka kuhamia Real Madrid. ***(Athletic)***

### MADRID YATOA MSIMAMO

ERLING Haaland mwenye umri wa miaka 21, anadaiwa hayuko katika mipango ya Real Madrid kwa sasa, huku klabu hiyo ya Hispania badala yake ikitaka kumsajili mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbape (23), ifikapo mwishoni mwa msimu huu. ***(El Chiringuito)***

### VLAHOVIC ALIIKATAA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 22, amesema ilikuwa uamuzi rahisi kuipuuza Arsenal na kujiunga na Juventus wakati wa dirisha la uhamisho la Januari. ***(Metro)***

### KOUNDE ANUKIA CHELSEA

KIUNGO wa kati wa West Ham mwenye umri wa miaka 23 na England, Declan Rice, beki wa kati wa Sevilla, Jules Kounde (23) na Aurelien Tchouameni (22), kutoka Monaco, wameorodheshwa na kocha wa Chelsea kama wachezaji wanaolengwa na timu hiyo mwisho wa msimu huu ***(Athletic)***

### NAPOLI YAIGOMEA NEWCASTLE

OMBI la Newcastle United la dau la pauni milioni 40 la kumsajili kiungo wa kati wa Napoli na Timu ya Taifa ya Hispania, Fabian Ruiz mwenye umri wa miaka 25 limekataliwa.***(Corriere dello Sport)***

### HOWE AMTAKA BOTMAN

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe atawasilisha ombi la kumsajili, Sven Botman mwenye umri wa miaka 22, mwishoni mwa msimu huu baada ya kumkosa beki huyo wa Lille na Uholanzi kwa dau la pauni milioni 35. ***(Mirror)***

### CARVALHO KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL ina matumaini ya kukamilisha usajili wa mapema wa mshambuliaji wa Fulahm, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 19, kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Sports)***

### ZAPATA ALIOTA MBAWA

KLABU ya West Ham ilishindwa katika siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho kumsaini mshambuliaji wa Colombia, Duvan Zapata mwenye umri wa miaka 30 kwa mkopo kutoka klabu ya Italia, Atalanta. ***(Sky Sports)***

### DEMBELE KITAELEWEKA

RAIS wa Klabu ya Barcelona, Joan Laporta anaamini winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, amekubali kufikia mkataba na klabu nyingine kama mchezaji huru mwisho wa msimu huu. ***(Goal)***

### GIL ALITAKIWA HISPANIA

WINGA wa Hispania, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 20 amesema familia yake ilimtaka kurudi Hispania kuichezea Valencia kwa mkopo miezi sita tu baada ya kujiunga na Tottenham Hotspur. ***(Sun)***

### LEWIS : SIENDI KOKOTE

MLINZI wa Newcastle United, Jamal Lewis mwenye umri wa miaka 24 anadaiwa kukataa ombi la kuhamia katika klabu ya Stoke City na Birmingham City. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG: KUONDOKA ARSENAL KUMENIUMA SANA

Asema klabu hiyo itaendelea kubakia kwenye moyo wake kwa kipindi...

**LONDON, England**

PIERRE-Emerick Aubameyang ameumizwa na kuondoka kwake Arsenal lakini amesisitiza mara zote "nilijitoa kwa asilimia 100 kwa ajili ya kuipigania klabu."

Jumanne Arsenal ilitangaza Aubameyang ameondoka kwenye Uwanja wa Emirates kwa maelewano ya pande zote mbili.

Alijiunga na Barcelona kwa uhamisho huru, ingawa taarifa kamili juu ya uhamisho huo hazijawekwa wazi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kwa mara ya mwisho alichezea Arsenal Desemba 6, mwaka jana na alipokonywa unahodha na kuwekwa nje na kocha, Mikel Arteta kutokana na utovu wa nidhamu.

Baada ya Arsenal kuthibitisha kuondoka, Aubameyang aliposti katika mtandano wake wa Instagram: "Kwa mashabiki wa Arsenal, asante kwa kuifanya London kuwa nyumbani kwangu na familia yangu kwa miaka minne iliyopita. Tumepitia mabonde na milima pamoja, na sapoti yenu ina maana kubwa kwangu.

"Kupata nafasi ya kushinda mataji na heshima ya kuwa nahodha wa klabu hii ni kitu ambacho kitaishi kwenye moyo wangu milele.

"Mara zote nilijitoa kwa asilimia 100 kwa klabu na kufanya kila niliweza, lakini kuondoka kabisa bila kusema kwaheri maalumu inaniumiza sana, lakini hii ndio soka.

"Nina huzuni sikupata nafasi ya kuwasaidia wachezaji wenzangu kwa wiki chache zilizopita, lakini zina cha ziada lakini ni kuiheshimu klabu hii na kuwatakia mafanikio makubwa kwa siku zijazo! Nawapenda sana, Auba."

Aubameyang alifunga mabao 92 katika mechi 162 kwenye mashindano yote kwa Arsenal baada ya kujiunga nao kutoka Borussia Dortmund Januari, mwaka 2018.

Alishinda kiatu cha dhahabu kwa ufungaji bora kwenye Ligi Kuu England msimu wa 2018-19, pamoja na Mohamed Salah na Sadio Mane.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 896

MECHI KALI
CAMEROON
VERSUS
EGYPT
1 | 2.19
X | 2.92
2 | 3.71

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ALLI AMSHUKURU POCHETTINO BAADA YA KUONDOKA SPURS



**LIVERPOOL, England**

NYOTA mpya wa Everton, Dele Alli ametoa ujumbe wa shukrani maalumu kwa kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino baada ya kukamilisha uhamisho wa kwenda Goodison Park katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili.

Miaka saba ya Alli ya kukaa Tottenham ilifikia mwisho Jumatatu na kwenda Everton kwa uhamisho huru wa awali.

Everton watatakiwa kulipa pauni milioni 10 kwa kiungo huyo baada ya kucheza mechi 20, ambapo itategemea na kiwango chake na ada inaweza kupanda hadi pauni milioni 40.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alifunga mabao 67 na asisti 55 katika mechi 269 pale Spurs, akiwa alihamia hapo akitokea MK Dons mwaka 2015.

Alli aliamua kuposti ujumbe maalumu Jumanne kwa kuishukuru klabu yake ya zamani, akisema "mara zote" itakuwa moyoni mwake.

"Huu ndio ukurasa wa mwisho, lakini sio kitabu," aliandika. "Asante kwa ujumbe wenu.

"Nataka kumtaja rasmi Mauricio (Pochettino) na benchi lake la ufundi kwa kuniwezesha kuwa kwenye kiwango hiki tangu walipokea kwa mara ya kwanza pale Spurs.

# Laporta ashangaa Dembele kubaki Barca

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta ameshangaa, Ousmane Dembele kuamua kubaki kwenye klabu hiyo hadi mwisho wa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa Jumatatu, alikuwa akihusishwa na klabu mbalimbali baada ya kushindwa kufikia muafaka kuhusu mkataba wake.

Katika harakati za kutotaka kumwachia aondoke huru majira ya joto yajayo ili kupunguza mzigo wa mishahara.

Paris Saint Germain na Chelsea zilikuwa tayari kumsajili kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili, lakini dili hilo likashindikana.

Na sasa Laporta ameibuka na kumkosoa Dembele kwani haileti maana ya yeye kubaki kwenye klabu hiyo na akasema; "Tulimpa mapendekezo mawili na yalikuwa mazuri, lakini tunashangaa hakuyakubali.

"Moja lilikuwa kutoka kwenye klabu ya Uingereza, lakini hakutaka kwenda alichagua kubaki hapa kwa miezi sita, si vyema yeye kubaki kwenye klabu, kwa sababu kusaini kwake mkataba mpya ingetupa ahueni ya bajeti ya mishahara.

"Timu ya Dembele ni ngumu kuielewa, Xavi anafanyia kazi kwa ajili ya msimu ujao, tulifikiria kuwa Dembele ameshakubaliana na klabu nyingine, hivyo ndivyo wakala wake alivyotuambia," alisema Laporta.



,686,220

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/02/22 | 18:00 | Hull City vs Preston | 2.55 | 3.25 | 2.80 |
| 02. 05/02/22 | 18:30 | Maritimo vs GD Estoril | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 03. 05/02/22 | 19:00 | St Etienne vs Montpellier | 2.57 | 3.31 | 2.67 |
| 04. 05/02/22 | 20:30 | Swansea vs Blackburn | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 05. 05/02/22 | 21:00 | Pacos Ferreira vs Portimonense | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 06. 05/02/22 | 23:00 | Twente vs Vitesse Arnhem | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 07. 06/02/22 | 16:00 | Valencia vs Real Sociedad | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 08. 06/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Galatasaray | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 09. 06/02/22 | 16:00 | Amorebieta vs Real Oviedo | 2.79 | 3.04 | 2.55 |
| 10. 06/02/22 | 17:00 | Sampdoria vs Sassuolo | 2.81 | 3.56 | 2.36 |
| 11. 06/02/22 | 18:15 | Barcelona vs Atletico Madrid | 2.40 | 3.26 | 2.97 |
| 12. 06/02/22 | 20:00 | Udinese vs Torino | 2.86 | 3.21 | 2.51 |
| 13. 06/02/22 | 20:30 | Betis vs Villarreal | 2.33 | 3.44 | 2.94 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 03/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2182 | Onduparaka FC vs Kampala City Council | 6.17 | 3.66 | 1.50 |
| 16:00 | 1986 | Hadiya Hosahina FC vs Jimma Aba Jifar | 1.79 | 3.22 | 4.33 |
| 16:00 | 5001 | Shabab Al Dhahiriya vs Shabab Alsamu | 2.45 | 3.51 | 2.45 |
| 16:30 | 1035 | PS Tni vs Bali Utd Pusam | 4.64 | 3.38 | 1.70 |
| 16:30 | 1406 | Paradou AC vs CS Constantine | 2.38 | 2.78 | 3.12 |
| 17:00 | 3331 | Mumbai City FC vs ATK Mohun Bagan | 2.20 | 3.42 | 2.84 |
| 18:00 | 4046 | Doxa Katokopia vs Ethnikos Achnas | 1.71 | 3.52 | 4.34 |
| 18:00 | 5756 | Rio Ave U23 vs Benfica U23 | 4.43 | 3.61 | 1.67 |
| 18:15 | 1641 | Atromitos vs Lamia | 2.08 | 3.01 | 3.80 |
| 19:00 | 1670 | Mosaset AL Bireh vs Thagafi Tulkarem | 3.76 | 3.18 | 1.93 |
| 19:00 | 2648 | Anorthosis Famagusta vs Pafos FC | 1.76 | 3.22 | 4.52 |
| 19:00 | 3142 | Bahir Dar Kenema FC vs Saint George FC | 3.62 | 2.85 | 2.11 |
| 19:00 | 3347 | Simba vs Tanzania Prisons | 1.25 | 4.73 | 11.59 |
| 19:30 | 2332 | Jazira Abu Dhabi vs AS Pirae | 1.01 | 17.32 | 76.96 |
| 20:00 | 3788 | USM Alger vs JS Kabylie | 1.59 | 3.42 | 5.59 |
| 20:00 | 3981 | Potenza SC vs Foggia | 2.92 | 3.16 | 2.43 |
| 20:00 | 4278 | Avellino vs Juve Stabia | 1.82 | 3.42 | 4.36 |
| 21:00 | 1873 | CD Trofense vs Porto B | 2.61 | 3.15 | 2.61 |
| 21:00 | 2224 | Monte Azul SP vs Atibaia SP | 4.62 | 3.17 | 1.76 |
| 21:30 | 3669 | Resende RJ vs Portuguesa RJ | 3.13 | 3.09 | 2.19 |
| 21:30 | 4186 | Luziania DF vs Ceilandia Esporte Clube DF | 6.95 | 4.15 | 1.40 |
| 22:00 | 1187 | Cameroon vs Egypt | 2.19 | 2.92 | 3.71 |
| 22:00 | 1244 | La Equidad vs Rionegro Aguilas | 1.95 | 3.18 | 3.67 |
| 22:00 | 1300 | Manchester City W vs Tottenham W | 1.23 | 5.62 | 9.11 |
| 22:00 | 3278 | Real Sociedad vs Betis | 2.01 | 3.41 | 3.51 |
| 22:45 | 3385 | Eupen vs Anderlecht | 4.90 | 4.12 | 1.57 |
| 23:15 | 3118 | Sporting Farense vs Academica | 1.67 | 3.61 | 4.78 |
| 23:30 | 4975 | Athletic Bilbao vs Real Madrid | 2.85 | 3.23 | 2.41 |

IJUMAA - 04/02/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1324 | AD Guanacasteca vs AD Grecia | 2.44 | 3.21 | 2.64 |
| 00:05 | 1074 | Union Magdalena SM vs Deportivo Pasto | 2.30 | 3.13 | 2.89 |
| 01:00 | 3178 | Aimore RS vs Caxias RS | 2.76 | 2.95 | 2.51 |
| 01:00 | 5336 | Mirassol SP vs Guarani SP | 2.22 | 3.03 | 3.13 |
| 01:00 | 5650 | Ituano SP vs Inter De Limeira SP | 2.04 | 3.07 | 3.50 |
| 02:10 | 1983 | Jaguares de Cordoba vs Patriotas FC | 1.77 | 3.47 | 4.04 |
| 02:15 | 2933 | Fluminense vs Audax Rio EC RJ | 1.22 | 5.41 | 10.63 |
| 03:00 | 1678 | Guadelupe FC vs AD San Carlos | 2.60 | 3.23 | 2.46 |
| 03:30 | 4786 | Juventude RS vs Novo Hamburgo | 1.22 | 4.84 | 13.56 |
| 03:30 | 5422 | Bragantino SP vs Sao Paulo | 2.50 | 2.98 | 2.74 |
| 04:15 | 5928 | Atletico Nacional vs Deportes Tolima | 1.70 | 3.28 | 4.83 |
| 05:00 | 3935 | CS Cartagines vs Sporting San Jose | 1.40 | 4.72 | 5.78 |
| 11:45 | 2339 | Adelaide United vs Sydney FC | 2.91 | 3.46 | 2.26 |
| 16:35 | 2812 | Al Arabi Doha SC vs Al-Shamal | 1.46 | 4.45 | 5.23 |
| 16:35 | 5620 | Al Ahli Doha SC vs Al Khoor | 1.69 | 3.72 | 4.16 |
| 17:00 | 4683 | Kerala Blasters FC vs Northeast United FC | 1.25 | 5.23 | 9.29 |
| 18:30 | 5714 | CS Mioveni vs Voluntari | 2.59 | 2.93 | 2.83 |
| 18:45 | 2826 | Umm-Salal SC vs Qatar SC | 2.74 | 3.37 | 2.28 |
| 19:00 | 1393 | Wolfsberger AC vs Floridsdorfer AC | 1.24 | 5.60 | 8.89 |
| 20:00 | 1463 | Nieciecza KS vs Jagiellonia | 2.84 | 3.22 | 2.29 |
| 20:00 | 2556 | Slaven Belupo vs HNK Sibenik | 1.90 | 3.37 | 3.61 |
| 20:00 | 2622 | Kayserispor vs Hatayspor | 2.36 | 3.25 | 2.91 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# YACOUBA, KIBWANA, NINJA WAREJEA KUICHEZEA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Yanga waliokuwa majeruhi kwa muda mrefu, Yacouba Songne, Kibwana Shomari na Abdallah Shaibu 'Ninja' wameanza mazoezi ya pamoja na wenzao tayari kurejea dimbani kuitumikia timu hiyo inayopambana kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA.

Msemaji wa Yanga, Haji Manara, alisema wachezaji hao wamerejea kikosini baada ya kupona kufuatia miili yao kuimarika kutokana na matibabu sahihi ya nje ya nchi waliyopata.

"Ninja, Kibwana na Yacouba wameanza mazoezi ya viungo, kwa hiyo lile wimbi la wachezaji majeruhi katika timu yetu linaanza kupungua siku hadi siku. Huu ndiyo mpira, kwenye klabu ni lazima kutakuwa majeruhi, matibabu ya upasuaji yanakuwa ni kawaida kwenye timu za mpira," alisema Manara. Wachezaji hao walipelekwa Tunisia kwa nyakati tofauti, kwa ajili ya matibabu zaidi, baada ya kupata majeraha kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaendelea.

Yacouba, raia wa Burkina Faso ndiye aliyekuwa mchezaji wa kwanza kupata majeraha yaliyomfanya kukaa muda mrefu msimu huu kwenye mechi ya Ligi Kuu kati ya Yanga dhidi ya Ruvu Shooting iliyochezwa Novemba 2, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kibwana na Ninja wao walipelekwa Tunisia Januari mwaka huu, baada ya kupata majeraha kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu na kuwafanya wakose michuano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu.

Wakati huo huo, Manara amesema wachezaji, Yannick Bangala na Djuma Shaaban walitarajiwa kuwasili leo wakitokea Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), walikokuwa wameitwa kwenye timu ya taifa, huku kipa namba moja Djigui Diarra naye anatarajia kuwasili wakati wowote akitokea kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) baada ya Mali kuondolewa.



Wachezaji wa Ihefu FC ya Mbeya wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi ya Championship dhidi ya Gwambina itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Gwambina ulioko Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Nyota Bara wafunika Championship

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA waliowahi kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na timu mbalimbali, hivi sasa wanashindana kusaka Kiatu cha Dhahabu katika Ligi ya Championship, ambayo hutoa timu zitakazopanda daraja na kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Amissi Tambwe, straika wa zamani wa Simba na Yanga ambaye kwa sasa anaitumikia DTB FC, amezidi kuliongoza kundi hilo akiwa na mabao 12 huku timu yake ikiwa kileleni na pointi 39 wakati nyota wa zamani mwingine wa Simba, Nicolaus Gyan akikamata nafasi ya pili akiwa na mabao 10.

Wakati akiichezea Simba Ligi Kuu 2017 hadi 2019, Mghana huyo alikuwa akicheza kama beki wa kulia, lakini kwa sasa akiwa na DTB anacheza nafasi ya straika ambayo alikuwa akiichezea kabla ya kujiunga na Simba, akitokea Ebusua Dwarfs ya Ghana.

Wachezaji wengine wanaofuatia katika orodha ya kupachika mabao katika ligi hiyo ni Warsha Machungwa wa Mwadui, Abiudi Mtambuku (Kitayosce), Danny Mrwanda (Kengold) na Edward Songo wa JKT Tanzania ambao kila mmoja amefunga magoli saba.

Samuel Kamuntu yeye amefunga mabao sita, akiwa naye aliicheza Ligi Kuu akiwa na JKT Tanzania na ameshuka nayo na bado anaendelea kuitumikia, huku straika wa zamani wa Azam, Andrew Simchimba naye akiwa na mabao sita, kwa sasa anaichezea Ihefu kwa mkopo, ingawa naye alikuwa kwenye kikosi hicho msimu uliopita ikiwa Ligi Kuu, kabla ya kuteremka daraja.

Michezo
Alhamisi Februari 3, 2022
Nipashe



## Aubameyang: Kuondoka Arsenal kumeniuma sana

# SIMBA SC, PRISONS MECHI YA KIBABE

●●●Mnyama atamba uteja basi kwa sababu amepata dawa ya...

**Saada Akida na Faustine Feliciane**

KISASI au kumaliza uteja, hayo ndio maneno kutoka kila upande kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya mabingwa watetezi, Simba dhidi ya Prisons itakayochezwa leo kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Makocha wa timu hizo wote kutoka nje ya nchi, Pablo Franco wa Simba kutoka Hispania na Mkenya Patrick Odhiambo anayeifundisha Prisons watakutana kwa mara ya kwanza tangu watue kwenye timu hizo.

Simba inashuka dimbani leo ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa bao 1-0 katika mechi yake ya mwisho dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Kagera lakini ikiwa na morali ya ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Dar City kwenye mchezo wa Kombe la FA (ASFC).

Wakati Simba ikisuasua, Prisons pia haina msimu mzuri kutokana na matokeo mabaya iliyopata katika mechi zake zilizopita, wao pia wakisonga mbele katika michuano ya Kombe la FA kwa kuiondoa Rhino Rangers ya Tabora.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema wamejiandaa vizuri kupambana kwa ajili ya kuhakikisha wanazibakisha pointi zote tatu katika mchezo huo dhidi ya Prisons lakini watashuka dimbani kwa tahadhari.

Matola alisema licha ya Prisons kuwa katika nafasi ya chini kwenye msimamo, haina maana timu hiyo 'mbovu sana' na anaamini watakapokutana nao watakuwa tofauti na michezo yao iliyotanguliwa.

"Tumejiandaa vizuri kuelekea mchezo wetu dhidi ya Tanzania Prisons, tumejipanga kufanya vizuri katika mechi hiyo kwa kuongeza umakini, tutaingia uwanjani kesho (leo) kwa ajili ya kutafuta pointi tatu."

"Tumepitwa pointi 10 na Yanga, hatuliangalii hilo zaidi ya kupambana ili kushinda mechi zetu, kupata pointi tatu kwa sasa ndio muhimu, tunatambua ligi ni mbio ndefu na bado kuna mechi nyingi mbele yetu, kikubwa ni kupambana kuchukua pointi tatu kutoka kwa Tanzania Prisons kwanza," alisema Matola.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema matokeo waliyoyapata katika mechi tatu za mwisho ni ya kawaida katika mpira duniani kote na anashangaa kwa hapa nchini imekuwa ni 'masemango' kwa upande wao.



Wachezaji wa kimataifa wa Simba kutoka Zambia, Rally Bwalya (kulia) na Clatous Chama wakikumbatiana kwa furaha katika mechi ya michuano ya Kombe la FA dhidi ya Dar City FC. Simba ilipata ushindi wa mabao 6-0. **PICHA: MTANDAO**

Rweyemamu alisema wanafahamu ukubwa na mafanikio ya timu yao ndio sababu ya kusemwa lakini wanaamini watarejea katika ushindani na hatimaye kulibakisha taji Msimbazi.

"Siku zote timu kubwa inapopoteza mchezo ndio inasemwa sana, haya yanayoendelea yanatokana na ukubwa wetu na mafanikio yetu, kwetu haya yanatupa hamasa ya kujipanga tena ili kuendelea kufanya vizuri katika michezo ya mbele," alisema Rweyemamu.

Aliongeza msimu uliopita pia timu yao ilipoteza mechi mbili mfululizo lakini mwisho wa msimu walichukua ubingwa kutokana na kikosi chao bora kupambana kwa ajili ya kurejesha furaha kwa mashabiki na wanachama wao.

"Tumejiandaa vyema, yaliyopita yamepita bado malengo yetu yapo pale pale, hatuna presha wala wasiwasi, tutacheza mchezo wetu tukifahamu kitu wanachokihitaji mashabiki wetu ni ushindi tu," alisema meneja huyo.

Kocha Msaidizi wa Prisons, Shabani Kazumba, alisema wanawaheshimu Simba kwa sababu ni mabingwa watetezi lakini wataingia uwanjani kupambana kutafuta pointi tatu muhimu.

Alisema watacheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu Simba ni bora licha ya kusuasua katika baadhi ya mechi zake, hivyo wanahitaji kuongeza umakini katika mchezo huo.

"Kuwa nafasi ya chini haina maana tuko vibaya, nina imani anayechanga karata zake ndio atakayepata matokeo mazuri," alisema Kazumba.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Ruvu Shooting dhidi ya Mbeya Kwanza, ambapo Kocha wake Msaidizi, Nizar Khalfani, alisema kikosi chake kiko katika hali nzuri na kimejiandaa kupata matokeo chanya.

## Nabi na hesabu kulisogelea taji

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anafurahi kuona kikosi chake kimeendelea kuimarika kwa ajili ya kuhakikisha wanatimiza malengo ya kuibuka na ushindi katika mchezo wao dhidi ya Mbeya City utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Tayari Mbeya City imeshawasili jijini kwa ajili ya kuwakabili vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao mpaka sasa hawajapoteza mechi hata moja.

Nabi aliliambia gazeti hili 'hesabu zake' kuelekea mechi hiyo zinakwenda vyema na kila mchezaji anaonekana yuko tayari kuisaidia timu ipate ushindi.

Hata hivyo, Nabi alisema wachezaji wake wanatakiwa kuongeza umakini kufuatia baadhi ya matukio anayoyaona wanapokuwa katika mazoezi kwa sababu anafahamu wapinzani wao pia wamejipanga.

Kocha huyo alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha msimu huu wanabeba ubingwa kwa sababu hiyo kwao kila mechi wanayocheza ni sawa na fainali.

"Kikubwa ambacho tunahitaji ni pointi tatu muhimu, ili kupata pointi ni lazima tushinde mchezo wetu. Ushindani ni mkubwa na kila timu inafanya kazi kubwa kusaka pointi, kazi ni kubwa na wachezaji watahakikisha wanatekeleza kile tunachokifundisha kwenye mazoezi kwa kukipeleka uwanjani," alisema Nabi.

Alisema wapinzani wao wamekuwa na kikosi imara zaidi msimu huu na wamejiandaa kukutana na ushindani mkubwa katika mechi hiyo kutokana na mabadiliko yaliyofanywa kwenye kikosi chao.

"Tunazihitaji pointi, nimeandaa kikosi changu kwa ajili ya kupata matokeo mazuri, hakuna mechi ndogo, hakuna timu ndogo, ligi hii ni ngumu, kikubwa ni kuongeza utulivu ili kujiimarisha katika mbio za ubingwa, tunapokuwa na mpira na kujipanga pale unapokuwa kwa wapinzani wetu, " Nabi aliongeza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >